# Nipashe

Jumatano Aprili 15, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580206

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US


**JIKINGE NA MARADHI MBALIMBALI IKIWEMO COVID-19 KWA KUTUMIA 'AMAZING GREEN SOIL', DKT ASHAURI**




Dr.Riser Nitsch from Muenster University, Germany

SOMA UK: 2



## CAG abaini upotevu mabilioni ya fedha vitambulisho vya Nida

UKURASA 3

# Shule, vyuo nchini kuendelea kufungwa

- **Serikali** yasitisha sherehe za maadhimisho Mei Mosi, Muungano... *Endelea ukurasa 8*



**BAA LA CORONA**

**Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO), mpaka jana jioni idadi ya watu waliopata maambukizi ya virusi vya corona maeneo mbalimbali duniani ni 1,844,863, vifo vilivyothibitishwa ni 117,021 na nchi zilizoathirika ni 213.**
- **Epuka mikusanyiko ya watu**
- **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
- **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**



Kijana (mwenye fulana nyeusi), akisimamia watu kuvuka Mto Ng'ombe, kwa kutumia viroba vyenye mchanga alivyovipanga kwenye maji, katika eneo la Magomeni maarufu kwa Mzee wa shamba kwenda Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana, ambapo mtu mmoja hutozwa Sh.500 kuvuka. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Mil. 297/- zaokolewa ununuzi wa nondo


UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

## Wahudumu wa baa lazima kuvaa barakoa

UKURASA 2


**MICHEZO** **SIMBA KUIBURUZA YANGA FIFA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# TCRA kuibana mitandao kijamii

**Na Mwandishi wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imewataka wananchi kupiga picha (Screen short) ujumbe wowote katika mitandao ya kijamii unaopotosha kuhusu corona na kuwatumia.

Ujumbe huo ni uliosambazwa kwenye makundi songezi na mmoja wa wanakundi, ili kuweza kuwachukulia hatua zaidi.

"Ukipokea au ukiona ujumbe unaochochea, kuzusha au kupotosha taarifa za corona katika group (kundi) lako au lolote lingine mtandaoni, piga picha ujumbe huo na namna ya aliyetuma na utume TCRA," lilisema tangazo hilo. Aidha, tangazo hilo linakuja siku chache baada ya tangazo la awali la kuwaonya wanaosambara taarifa au picha za masuala ya corona kwenye mitandao ya kijamii atachukuliwa hatua.

Machi 27, mwaka huu, Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, liliwakamata mume na mke kwa kutoa taarifa za uongo na kejeli kwa Serikali kuhusu janga la korona.

Hivi karibuni, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema kuna mtu mmoja alikamatwa kwa kutoa tangazo la kuongeza kwa muda wa shule kufungwa, huku akieleza kuwa hatua zitaendelea kuchukuliwa kwa wanaosambaza taarifa za uzushi.

Machi 16, Tanzania ilithibitisha kisa cha kwanza cha mgonjwa wa Corona, Isabella Mwampamba (46), aliyetokea nchini Ubelgiji na kutua katika Uwanja wa Ndege wa KIA mkoani Kilimanjaro.

Isabella aliwasili Tanzania Machi 15, kupitia uwanja huo akitokea Ubelgiji na alikaguliwa uwanjani hapo lakini hakugundulika kuwa na homa kuashiria ugonjwa huo.

Lakini, baada ya kutoka uwanjani hapo alianza kujisikia vibaya ndipo alipoamua kwenda hotelini kujitenga na familia yake kisha kwenda hospitali kufanyiwa matibabu ndipo alipogundulika kuwa na virusi hivyo.

Msafiri huyo aliondoka nchini Machi 3, mwaka huu ambapo kati ya Machi 5 hadi Machi 13, alitembelea nchi za Sweden na Denmark na kurudi tena Ubelgiji.

Machi 31, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto, ilitangaza kifo cha kwanza cha Mtanzania mwenye umri wa miaka 49 kufariki kwa corona ambaye pia alikuwa akisumbuliwa na maradhi mengine.

Hadi sasa, waliofariki dunia kwa ugonjwa huo ni watu watatu wote wakiwa ni wanaume na wanaougua hadi juzi walikuwa ni watu 49.

Machi 17, serikali ilitangaza kufunga shule zote kuanzia za awali hadi kidato cha sita kwa siku 30 ikiwa ni hatua ya kuzuia kuenea kwa maambukizi ya ugonjwa huo.

Aprili 12, Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), ilitangaza kuanzia Aprili 11, ndege zote za kimataifa za abiria ambazo zilikuwa na ratiba ya kutua na hata ambazo hazikuwa na ratiba zinapigwa marufuku kutua.

Mikoa iliyotangazwa kuwa na watu wenye maambukizi ni Dar es Salaam, Arusha, Kagera na visiwani Zanzibar.

Corona ilianzia kwenye mji wa Wuhan China, mwishoni mwa Desemba mwaka jana, na kwa mujibu wa kituo cha utafiti cha Chuo Kikuu cha Johns Hopkins nchini Marekani, hadi jana jumla ya watu 1,934,583 wanaugua ugonjwa huo.

Aidha, watu 120,863 wameshafariki na nchi au maeneo ya utawala yenye maambukizi ni 185, huku nchi iliyoathirika zaidi ni Marekani yenye watu 582,634 wanaougua na kati yake 23,649 wamefariki.



Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Richard Kasesela (kushoto), akizungumza na wamiliki wa baa, mjini Iringa jana, kuhusu kuchukua tahadhari ya maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Wahudumu wa baa lazima kuvaa barakoa

**Na Waandishi Wetu**

MKUU wa wilaya ya Iringa, Richard Kasesela, ameagiza wamiliki wa baa kuhakikisha wafanyakazi wao wanavaa barakoa kwa ajili ya kujikinga na virusi vya corona.

Aidha, amtaka kila mmiliki wa sehemu zenye mikusanyiko ya watu kuhakikisha kuna maji yanayotiririka na sabuni kwa ajili ya watu kunawa.

Akizungumza na wamiliki wa baa, Mkuu huyo wa wilaya alisema ni muhimu wahudumu hao kuhakikisha wananawa mikono ikiwamo kutumia majitiba.

Aidha, alisema wilaya hiyo imejipanga vyema na iwapo itatokea mtu mwenye maambukizi hatua zitachukuliwa za kumtenga na kuwachukua na kuwatenga na jamii.

Kwa mujibu wa Kasesela, wamiliki hao wanapaswa kuhakikisha wateja na wahuduma wanakaa umbali uliopendekezwa na wizara ikiwa ni hatua ya kujikinga na maambukizi.

"Wale wote wanaokuwa kwenye maeneo ya burudani wanapaswa kukaa kwa umbali unaotakiwa na watakaokiuka watachukuliwa hatua kwa kufunga biashara zao," alisema.

Kwa kuonyesha mfano, Mkuu huyo wa wilaya ambaye alikuwa amevaa barakoa, alisema ni lazima watu kukaa kwa umbali wa mita moja, ikiwamo wapenzi kuhakikisha wanajitenga.

Kuhusu muda wa kufunga baa, Kasesela alisema Manispaa hiyo itaangalia muda wa kufunga kwa kuwa wapo wanaoendelea kufanyabiashara hadi usiku wa manane.

Aidha, alisema anakusudia kukutana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na wafanyabiashara mkoani humo kujadili suala hilo.

**MBUNGE MARUFUKU WATU KWENDA BAA**

Wakati huo huo, Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Ruth Mollel, alishauri kupigwa marufuku watu kwenda baa na kuweka ulazima wa kuvaa barakoa kwenye maeneo yote yenye msongamano wa watu.

Akichangia jana Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(Tamisemi) mwaka 2020/21, walipongeza hatua zilizochukuliwa na serikali na kusisitiza hatua zaidi zichukuliwe ili kudhibiti maambukizi ya ndani.

Mollel alisema ni vyema serikali ikapiga marufuku watu kwenda baa au vijiweni kwa kuwa ni sehemu zinazochochea maambukizi ya ugonjwa huo.

"Kwanini serikali isipige marufuku watu kwenda baa? Kwenda kwenye vijiwe ni sehemu ambayo inachochea maambukizi, watu wanunue vinywaji vyao wanywee nyumbani na wasikusanyike mahali," alisema.

Alibainisha kuwa, kutokana na corona kuonekana kuambukiza kwa njia ya hewa, kuna mahitaji ya kuvaa barakoa licha ya kwamba hazipatikani.

**Imeandikwa na Francis Godwin, IRINGA na Augusta Njoji, DODOMA**

## CAG abaini tatizo ujenzi jengo la ghorofa 10 CCM

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini dosari katika utekelezaji wa mradi wa ubia wa ujenzi wa bandari kavu (ICD), ulioanzishwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2018/19, CAG Charles Kichere, anasema mradi huo haujatekelezwa.

CAG anasema katika mapitio ya nyaraka za CCM, alibaini makubaliano ya ubia na moja ya kampuni yaliyokuwa na lengo la ujenzi wa ICD, jengo la ghorofa 10 na lingine la ghorofa nne kwenye viwanja tofauti vinavyomilikiwa na CCM, vilivyoko Mkoa wa Dar es Salaam Julai 2015.

"Kulingana na makubaliano hayo, ujenzi ulipangwa kukamilika ndani ya kipindi cha miaka mitatu; na kwamba kampuni tajwa itagharamia mradi wote kwa gharama iliyokadiriwa ya Sh. 17,958,565,557.96 (bilioni 17.958).

"Pia, nilibaini kuwa umiliki wa hisa kwenye mradi wa ubia ni asilimia 30 kwa CCM na asilimia 70 kwa kampuni tajwa. Kwenye makubaliano hayo, pia nilibaini kuwa kodi ya pango ya Sh. 5,000,000 (milioni tano) ilitakiwa kulipwa na kampuni tajwa kwenye Ofisi ya CCM ya wilaya ya Temeke.

"Hata hivyo, katika ukaguzi wangu wa mwezi Januari 2020, nilibaini hapakuwa na ujenzi uliokuwa unaendelea kwenye viwanja vyote vilivyotolewa na CCM kwa ajili ya mradi wa ubia na kampuni tajwa.

"Hata hivyo, kampuni tajwa haikulipa kodi ya pango ya jumla ya Sh. 80,000,000 kuanzia Machi 2018 hadi Juni 2018 kama walivyokubaliana kwenye makubaliano ya ubia," anabainisha.

CAG anasema ana shaka ya kuchelewa kutekelezwa kwa mradi huo kama walivyokubaliana kwenye mkataba wa ubia ambao umechelewesha CCM kupokea kiwango chake cha faida.

"Katika hili, ninapendekeza uongozi wa CCM kurejea upya mkataba wa ubia uliosainiwa ili kuendana na mahitaji mapya ya uwekezaji ambao unafanywa na CCM kwa sasa," CAG anashauri.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akiteta jambo na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, kwenye kikao cha Kamati ya Kitaifa ya Uratibu wa Mapambano dhidi ya Ugonjwa wa Homa kali ya Mapafu (COVID - 19), jijini Dodoma, jana. **PICHA: OWM**

# CAG abaini upotevu mabilioni ya fedha vitambulisho vya Nida

**Na Sanula Athanas,**
DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini dosari katika utoaji wa vitambulisho vya taifa unaofanywa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2018/19, CAG Charles Kichere, anasema mapitio ya takwimu za uzalishaji wa vitambulisho kwa Februari 2020, alibaini Nida iliandikisha watu 21,692,122 kati ya makadirio ya watu 24,008,729.

Hata hivyo, CAG anabainisha kuwa kati ya watu 21,692,122 waliandikishwa, ni watu 17,100,178 waliopatiwa nambari za vitambulisho vya taifa, huku idadi iliyobakia ya watu 4,591,944 (sawa na asilimia 21) ikiwa bado haijapata nambari hizo.

"Pia, nilibaini kuwa kati ya watu 17,100,178 waliopata nambari za vitambulisho vya taifa, ni kadi za watu 5,996,304 ndizo zilizotengenezwa huku idadi iliyobakia ya watu 11,103,874 wenye nambari za vitambulisho (sawa na asilimia 65) wakiwa bado hawajapata kadi za vitambulisho," anabainisha.

**UNUNUZI MTAMBO BIL. 8.3/-**

CAG anaongeza kuwa baada ya kubaini uzalishaji mdogo wa vitambulisho, alipitia uwezo wa mfumo wa uzalishaji wa kadi za vitambulisho na kugundua kwamba Nida ilifanya ununuzi wa mashine mpya ya chapa vitambulisho kutoka kwa M/s Atlantic Zeiser GmbH kwa gharama ya Euro 3,304,650 (Sh. bilioni 8.305) kupitia mkataba wenye nambari EA/061/2018-2019/HQ/G/01-Lot 3 wa Julai 22, 2019.

"Hata hivyo, mashine hiyo ilishindwa kufanya kazi kwa sababu bakaa ya kadi haikuendana na mfumo uliopo kwenye mshine hiyo ya chapa na hivyo kusababisha ugumu kwenye uzalishaji wa vitambulisho hivyo.

"Ni maoni yangu kwamba, ucheleweshaji wa utoaji wa nambari za vitambulisho vya taifa kwa raia wanaostahili, utazuia upatikanaji wa mawasiliano ya simu za mkononi kwa kuwa usajili wa laini za simu unataka mtumiaji kuwa na nambari ya kitambulisho cha taifa.

"Kukosekana kwake kumepelekea kampuni za simu kufuata maelekezo ya kuzifungia laini zote ambazo hazijasajiliwa kuanzia Januari 2020.

"Hivyo, napendekeza Menejimenti ya Nida kuharakisha mchakato mzima wa utoaji wa nambari za vitambulisho vya utaifa ili kuwezesha watumiaji wa simu za mkononi kufuata maagizo ya TCRA (Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano) ya kuhakikisha laini zote za simu zinasajiliwa," anashauri.

**BILIONI 28/-**

CAG pia anasema kwamba, Aprili 21, 2011, NIDA iliingia kwenye makubaliano ya kimkataba na IRIS Corporation Berhad ya Malaysia kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa na vifaa vya utekelezaji wa mfumo wa kadi za taifa kwa kutumia teknolojia ya kisasa kwa gharama ya Dola 149,956,303 kwa muda unaoishia Septemba 13, 2016; na baadae kusogezwa mpaka Machi 14, 2018.

Katika ukaguzi wa mkataba huo, CAG anasema alibaini mkandarasi alilipwa malipo ya awali yenye thamani ya Dola za Marekani 29,991,260 (sawa na Sh. 47,992,080,000) mnamo Septemba 16, 2011.

Hata hivyo, anasema ni kiasi cha Sh. 19,776,633,530 ndicho kilichorudishwa na mkandarasi mpaka muda wa ukaguzi wa Januari 2020, huku kiasi kilichobakia cha Sh. 28,215,446,470 (bilioni 28.215) kikiwa hakijarudishwa japokuwa mkataba uliisha muda wake tokea Machi 14, 2018 (miaka mwili nyuma).

"Pia, ukaguzi wangu wa ziada ulibaini kuwa mkandarasi alikuwa na madai ya kiasi cha Dola za Marekani 5,933,536.56 (sawa na Sh. bilioni 13.651), ambapo madai hayo hayatoshi kufidia kwa ujumla deni la malipo ya awali ya Sh. 28,215,446,470.

"Ni maoni yangu kwamba, udhaifu umetokana na usimamizi usioridhisha wa mkataba huu na NIDA. Hii inaweza kuchangia upotezaji wa fedha za mlipakodi pale ambapo hapatakuwa na njia madhubuti itakayosaidia upatikanaji wa fedha hiyo.

"Napendekeza kwa Menejimenti ya NIDA kufidia deni la malipo ya awali la Sh. 28,215,446,470 na madai ya mkandarasi yenye thamani ya Sh. 13,651,584,240.42 na kuhakikisha kiasi kilichobakia cha Sh. 14,563,862,229.58 kinakusanywa kutoka kwa mkandarasi. Pia, wizara mama (Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi) ifuatilie kuhakikisha mamlaka inakusanya deni hilo," anashauri.

**UPOTEVU WA VIFAA**

CAG pai anasema amebaini upotevu wa vifaa vinavyosaidia mashine za Biometrika za Uandikishaji wa Wapigakura (BVR).

Katika hilo, CAG anafafanua kuwa, NIDA ilianzisha ofisi kwenye wilaya mbalimbali na kuziwezesha kwa mashine mahususi za biometrika za uandikishaji wa wapigakura ili kusaidia katika shughuli za uandikishaji wa vitambulisho vya taifa.

Hata hivyo, anasema ukaguzi wake wa taarifa ya vifaa vya teknolojia ya mawasiliano na habari, ulibaini kuwa vifaa vilivyotolewa kwa ajili ya kutumika na mashine za BVR, vilipotea kwenye halmashauri mbalimbali.

"Menejimenti ilitaarifu ofisi yangu kuwa imewasiliana na Ofisi ya Rais-Tamisemi kuhusiana na vifaa vilivyoibiwa ambao ndiyo wana jukumu la kusimamia masuala ya Halmashauri za Wilaya.

"Hata hivyo, natambua ukosefu wa vifaa hivi unapunguza kasi ya shughuli za uandikishaji. Kwa hivyo, napendekeza NIDA ichukue hatua za haraka kuhakikisha upatikanaji mbadala wa vifaa vyote vilivyopotea ili kurejesha kasi ya uandikishaji.

"Pia, NIDA inashauriwa kuhakikisha usalama wa vifaa vya usajili na kuhakikisha hatua stahiki zinachukuliwa ili kurejesha vifaa vilivyopotea pamoja na hatua za kisheria zinachukuliwa kwa wahusika wa wizi," CAG anashauri.

# Mil. 297/- zaokolewa ununuzi wa nondo

**Na Manuel Kaminyoge,**
SONGWE

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoa wa Songwe, imeokoa zaidi ya Sh. milioni 297 kutoka kwenye mradi wa maji Iyula wilayani Mbozi kutokana na udanganyifu wa kutaka kuiibia Serikali.

Udanganyifu huo unadaiwa kufanywa na mkandarasi wa Kampuni ya Ujenzi ya STC Dar es Salaam na Mhandisi wa maji wilaya ya Mbozi walidanganya Serikali kwa kununua nondo ya milimita 10 kwa Sh. 78,000 badala ya 7,800 kwa kila nondo.

Kamanda wa Takukuru mkoa wa Songwe, Damas Suta, alisema katika mradi wa maji Iyula wilayani humo wenye gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 5.139.

Alisema mradi huo ulikutwa na kasoro za udanganyifu wa bei za nondo kuwa juu kuliko bei ya soko kwa wakati huo,katika ujenzi wa matanki ya maji ya Iyula A,Iyula 'B' na Senyele .

"Bei ya nondo kwa kilogramu moja aliweka kwenye makisio ya gharama za ujenzi ( BOQ )zisizokuwa na uhalisia wa bei za soko za kipindi husika, ambapo bei ya nondo ya milimita 10 iliandika Sh.78000,wakati bei halisi ya nondo hiyo ni MM10 sokoni kwa wakati huo ilikuwa ni 7,800 kwa kilogram" alisema.

Alisema mkandarasi huyo kwa kuzidisha huko kwa bei kulipelekea kuongezeka gharama ya mradi huo, hivyo kuisababishia Serikali hasara ya Sh. 297,961,092 , kiasi ambacho kama taasisi hiyo imeona ni kosa.

Kamanda suta alisema udanganyifu huo wa Mkandarasi ulifanikiwa kufanyika kutokana na uzembe wa aliyekuwa mkandarasi wa maji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kwa kipindi hicho pamoja na wataalamu walioshiriki kufanya tathmini ya zabuni hiyo kwa makusudi kufumbia macho udanganyifu wa kampuni hiyo ya STC Construction Company.

Siku chache zilizopita mkuu wa mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali Nicodemus Mwangela, baada ya kutembelea mradi huo aliagiza mkandarasi wa mradi wa maji wa Iyula uliopo Wilaya ya Mbozi kuzuiwa kutoka Nje ya Mkoa wa Songwe huku akiwekwa chini ya uangalizi wa jeshi la Polisi mpaka atakapo kamilisha vifaa na wataalamu watakaomalizia mradi huo.

## Mazungumzo Kigogo Takukuru, DPP yaendelea

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi inayomkabili Mkurugenzi wa zamani wa Mipango, Ufuatiliaji na Tathimini wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Kulthum Mansoor, umedai unaendelea na mazungumzo kati ya ndugu wa mshtakiwa huyo na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP).

Kadhalika, umedai kuwa mazungumzo hayo yameendelea baada ya mshtakiwa kumwandikia DPP barua ya kukiri makosa yake.

Kesi hiyo ilipangwa jana kwa ajili ya kutajwa mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Mfawidhi, Godfrey Isaya, anayesikiliza usikilizwaji wa awali wa kesi hiyo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, ndiye aliyetoa madai Jamhuri kuendelea na mazungumzo na mshtakiwa.

Kesi hiyo iliahirishwa bila mshtakiwa kuwapo mahakamani kutokana na ugonjwa wa corona, mahabusi wanaendelea kukaa gerezani, huku kesi zao zikiahirishwa kwa uwakilishi wa mawakili wa utetezi.

Mshtakiwa huyo ambaye anakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo mashtaka manane ya kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha fedha kiasi cha Sh. bilioni 1.477 kuingia kwenye majadiliano na DPP, lakini wakashindwa kuelewana na majadiliano hayo yalikufa Januari, 2020 na baadaye mchakato ulianza upya.

Ilidaiwa katika tarehe tofauti kati ya Januari 2013 na Mei 2018, mshtakiwa alighushi barua ya ofa ya Agosti 13, 2003 kwa madhumuni ya kuonyesha kuwa barua hiyo imetolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, huku akijua kuwa sio kweli.

Katika shtaka ya pili, inadaiwa kati ya Januari 2012 na Mei 2017 maeneo ya Upanga katika Wilaya ya Ilala, mshtakiwa kwa udanganyifu alijipatia Sh. milioni 5.2 kutoka kwa Alex Mavika, mfanyakazi wa Takukuru kama malipo ya kiwanja kilichopo Kijiji cha Ukuni Bagamoyo.

Pia inadaiwa kati ya tarehe hizo, Mansoor alijipatia Sh. milioni tatu kutoka kwa Katondo kama malipo ya kiwanja kilichopo maeneo ya Kijiji cha Ukuni wilayani Bagamoyo mkoani Pwani.

Mshtakiwa huyo pia alijipatia Sh. milioni tano kutoka kwa Ofisa wa Takukuru, Gogo Migutah kama malipo ya kiwanja kilichopo eneo hilo.

Katika shtaka la tano, inadaiwa Mansoor alijipatia Sh. milioni saba kutoka kwa Ekwabi Majungu, ofisa wa Takukuru kama malipo ya kiwanja hicho.

Mansoor anadaiwa kati ya Januari 2012 na Mei 2017, maeneo ya Upanga jijini Dar es Salaam, akiwa Mkurugenzi wa Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini alijipatia Sh. milioni saba kutoka kwa John Sangwa kama malipo ya kiwanja cha eneo hilo.

Inadaiwa mshtakiwa akiwa mwajiriwa wa Takukuru, alijipatia Sh. milioni tano kutoka kwa Rose Shingela kwa ajili ya malipo hayo.

Aidha, katika mashtaka ya utakatishaji fedha, mshtakiwa huyo anadaiwa kati ya Januari 2013 na Mei 2018 maeneo ya Upanga alijipatia Sh. 1,477,243,000 wakati akijua kuwa fedha hizo ni haramu na ni zao la kosa tangulizi la kughushi.

# Misaada ya corona yafikia bil. 6.726/-

**Na Mwandishi Wetu**

MISAADA ya kusaidia Serikali kukabiliana na janga la corona imeendelea kumiminika na kufikia zaidi ya Sh. bilioni 6.726, ikiwa ni fedha taslimu na vifaa.

Jana Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipokea hundi ya mfano ya Sh. milioni 500 kutoka kampuni ya Export Trading Group (ETG) kwa ajili ya kukabiliana na janga hilo linaloitafuna dunia.

Waziri Mkuu alipokea msaada huo jana ofisini kwake Mlimwa, jijini Dodoma, kutoka kwa Mkurugenzi mkazi wa ETG, Nilladri Chowdhury.

Wiki iliyopita Waziri Mkuu, pia alipokea zaidi ya Sh. milioni 6.226 kutoka kwa wadau mbalimbali nchini, kwa ajili ya maji tiba na barakoa za kuwasaidia wananchi na watumishi wa afya katika kukabiliana na janga hilo.

Akizungumza baada ya kupokea msaada huo, Waziri Mkuu aliwashukuru watendaji wa kampuni ya ETG kwa kuunga mkono juhudi za Serikali katika mapambano dhidi ya virusi vya corona, ambapo hadi sasa kesi 49 zimeripotiwa tangu kuanza kwa ugonjwa huo nchini na wagonjwa saba wameshapona.

"Kwa niaba ya Rais wetu, Dk. John Magufuli, tunawashukuru kwa msaada huu, ambao utaisaidia Serikali kupunguza makali ya kuwahudumia wananchi wetu. Tunahitaji kuungwa mkono na wadau wengine kama ninyi," alisema. Aliwataka wananchi wote wazidishe kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo hasa katika kipindi hiki.

"Hatua tuliyofikia hivi sasa, maambukizi yameanza kuongezeka hasa kwa Dar es Salaam na Zanzibar. Tunajua kule kuna watu wengi na shughuli zote za kiuchumi zinaanzia pale, lakini hatunabudi kufuata masharti tuliyopewa ili kuzuia ugonjwa huu usisambae," alisema.

"Serikali inatoa msisitizo kwa wananchi wazingatie maelekezo yanayotolewa kuhusu kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona ikiwamo kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka pamoja na kujiepusha na mikusanyiko isiyokuwa ya lazima."

"Muhimu zaidi sote tuendelee kumuomba Mwenyezi Mkungu ili atupunguzie makali ya ugonjwa huu," alisisitiza.

Awali, Mwenyekiti wa Kampuni ya ETG, Mahesh Patel, Mkurugenzi Mkazi wa ETG, Nilladri Chowdhury, alisema wameamua kuchangia ili kuunga mkono juhudi za Serikali katika vita ya kupambana na ugonjwa huo.

Alisema kampuni yao inashughulika na masuala ya kilimo ikiwamo kusambaza pembejeo na kuongeza thamani mazao kupitia kampuni yao ya Kapunga iliyoko Mbeya, viwanda vitatu vya kubangua korosho vilivyoko Mtwara, Newala na Tunduru na viwanda vya kusindika mbegu za mafuta.

Pia, wanatoa soko kwa wakulima kwa kununua mazao kama korosho, mbaazi, kokoa, mahindi, choroko na ufuta.

Corona ilianzia kwenye mji wa Wuhan China, mwishoni mwa Disemba mwaka jana, na kwa mujibu wa kituo cha utafiti cha Chuo Kikuu cha Johns Hopkins nchini Marekani, hadi jana jumla ya watu 1,934,583 wanaugua ugonjwa huo.

Aidha, watu 120,863 wameshafariki na nchi au maeneo ya utawala yenye maambukizi ni 185, huku nchi iliyoathirika zaidi ni Marekani yenye watu 582,634 wanaougua na kati yake 23,649 wamefariki.



Mkazi wa mji wa Morogoro, Masungwa Kaseka, akiwa na bango lenye ujumbe wa kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona, jana. Kaseka alisema kuwa ameanza ziara ya kutembea mkoa mzima kwa miguu, kwaajili ya kufikisha ujumbe kwa jamii juu ya kujikinga na ugonjwa huo, huku yeye mwenyewe akionekana kutochukua tahadhari yoyote ikiwa ni pamoja na kutovaa Barakoa. **PICHA: FRANK KAUNDULA**

# Wilfred Lwakatare aliaga Bunge kwa ujumbe mzito

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKATI Mkutano wa 19 wa Bunge ukiendelea hadi jana, wabunge watatu kutoka Mkoa wa Kagera wameaga rasmi kutojihusisha na siasa.

Wabunge hao ni pamoja na Mbunge wa Muleba Kusini (CCM), Prof.Anna Tibaijuka, Mbunge wa Kuteuliwa, Abdallah Bulembo huku Mbunge wa Bukoba mjini(Chadema), Wilfred Lwakatare akiwa wa kwanza kutoka upinzani kuaga kutogombea.

Akichangia jana bungeni, Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), kwa mwaka 2020/21, Lwakatare, alisema: "Leo na mimi natangaza kufuata nyayo za Mama Tibaijuka na Bulembo, wote wa kule kule ukanda wa Kagera, napumzika katika siasa ambayo nimeitumikia kwa miaka mingi na kutumikia nafasi nyingi."

Alisema Tamisemi amekuwa mtumishi kwa muda wa miaka 13 akiwa Ofisa wa Utumishi na Utawala.

"Nikaingia kwenye siasa na nikailipa serikali mishahara mitatu nikabahatika kuwa mbunge na mwaka 2000 kuwa kiongozi wa kambi ya upinzani, lakini nikatumikia vyama vya CUF Naibu Katibu Mkuu na nikaenda Chadema kama Mkurugenzi wa ulinzi na inteligensia," alisema.

Alisema aligombea tena akashindwa, lakini akarudi tena mwaka 2015 na kumuondoa Mbunge wa wakati huo, Balozi Khamis Kagasheki.

"Sina deni na niliogombea nao, sina deni lolote na waliowahi kunishinda na niliowashinda, sina deni lolote, naamini nimejenga upinzani makini na naacha upinzani makini, ambao wanaweza kuongoza Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba," alisema. Alishukuru halmashauri hiyo kwa kufanya kazi bila mgogoro.

"Nishukuru kabisa madiwani wa Bukoba wa vyama vyote kwa kuwa tumeendesha halmashauri tukiwa tunaheshimiana na viongozi wa serikali akiwamo Mkuu wa Mkoa, nashukuru Mungu kwa kufika hatua hii," alisema.

Aliongeza: "Dk.Bashiru (Katibu Mkuu wa CCM) aliwahi kusema kinachokosekana nchi hii ni upinzani credible (unaoaminika), mimi nategemea upinzani credible unategemea na mpanga mipango awe credible kama hayupo credible upinzani hauwezi kuwa credible."

Lwakatare alimtaka Waziri wa Tamisemi, Selemani Jafo, kujipima katika uchaguzi anaosimamia kama ni halali na kama haupo halali hata upinzani hauwezi kuwa halali.

"Nawasikitikia Chama Cha Mapinduzi kuwa mmepata fursa ya kuongoza mabadiliko ya vyama vingi, tulitegemea ni upambanishaji wa fikira, tumeona nchi zingine wanapata faida kubwa... uchaguzi wa serikali za mitaa tuna viongozi ambao hawakubaliki kwa wananchi," alisema.

Alisema kuna baadhi ya waliochaguliwa wameona mambo hayaendi na wameanza kujiondoa.

# Taarifa ya fedha iliyokaguliwa

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### Waraka mizania kwa tarehe 31 Desemba 2019 (kiasi kwa shilingi milioni)

| A. Mali | Mwaka wa sasa 31/12/2019 | Mwaka uliyopita 31/12/2018 |
|---|---|---|
| 1. Fedha Taslimu | 25,996 | 27,363 |
| 2. Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 65,650 | 186,614 |
| 3. Uwekezaji katika amana za serikali | 151,218 | 125,143 |
| 4. Salio katika benki nyingine na taasisi za fedha | 191,791 | 90,836 |
| 5. Hundi na miamala ya kushughulikiwa | 720 | 1,091 |
| 6. Miamala baina ya matawi | - | - |
| 7. Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8. Dhima za wateja zilizokubalika | 53,065 | 30,952 |
| 9. Mikopo Iliyotolewa kwa benki nyingine | - | - |
| 10. Uwekezaji katika amana nyingine | 2,000 | - |
| 11. Mikopo halisi iliyopo | 465,899 | 459,667 |
| 12. Mali nyingine | 34,343 | 20,024 |
| 13. Uwekezaji wa hisa | - | - |
| 14. Akaunti za udhamini | - | - |
| 15. Mali zisizohamishika, mitambo na vifaa | 18,813 | 20,980 |
| **16. Jumla ya mali** | **1,009,496** | **962,670** |

| B: Dhima | Mwaka wa sasa 31/12/2019 | Mwaka uliyopita 31/12/2018 |
|---|---|---|
| 17. Amana za benki nyingine na taasisi za fedha | 51,296 | 125,252 |
| 18. Amana za wateja | 691,892 | 605,690 |
| 19. Dhamana ya malipo kwa fedha taslimu | 41,305 | 68,032 |
| 20. Amana maalumu | - | - |
| 21. Maagizo ya malipo/fedha za kuhamisha | - | - |
| 22. Hundi na hawala za kibenki zilizotolewa | 21 | 24 |
| 23. Limbiko la kodi na gharama zitakazolipwa | 3,603 | 3,921 |
| 24. Dhima la tozo kwa ajili ya usuluhishi Baina ya benki na mteja | 53,065 | 30,952 |
| 25. Miamala isiyoshughulikiwa baina ya matawi | - | - |
| 26. Mapato yaliyoingia ya kipindi kijacho na tozo Nyingine zitakazolipwa baadae | 2,517 | 3,697 |
| 27. Dhima nyingine | 20,355 | 2,740 |
| 28. Madeni | 22,173 | 15,133 |
| **29. Jumla ya dhima** | **886,227** | **855,441** |
| **30.Mali/(dhima) halisi (16 minus 29)** | **123,269** | **107,229** |

| C. Fedha za wanahisa | Mwaka wa sasa 31/12/2019 | Mwaka uliyopita 31/12/2018 |
|---|---|---|
| 31 Mtaji wa hisa uliolipwa | 92,432 | 85,270 |
| 32. Akiba ya mtaji | 76 | 76 |
| 33. Mapato yaliyobakizwa | (9,210) | (18,845) |
| 34. Faida/(hasara) ya kipindi husika | 9,616 | 6,030 |
| 35. Akaunti nyingine za mtaji | 30,355 | 34,697 |
| 36. Stahiki ya wenye hisa chache | - | - |
| 37. Jumla ya fedha za wanahisa | 123,269 | 107,229 |
| 38. Dhima zisizo dhahiri | 119,852 | 131,148 |
| 39. Mikopo chechefu | 18,066 | 15,405 |
| 40. Tengo kwa ajili ya mikopo chechefu | 21,680 | 20,259 |
| 41. Mali nyingine chechefu | - | - |

| D. Baadhi ya viashirio vya hali ya kifedha | Mwaka wa sasa 31/12/2019 | Mwaka uliyopita 31/12/2018 |
|---|---|---|
| (i) Uwiano wa fedha za wanahisa na jumla ya mali | 12.2% | 11.1% |
| (ii) Uwiano wa mikopo chechefu na jumla ya mikopo ghafi | 3.9% | 4.3% |
| (iii) Uwiano wa mikopo ghafi na jumla ya amana | 66.5% | 71.3% |
| (iv) Uwiano wa mikopo halisi na jumla ya mali halisi | 46.2% | 47.7% |
| (v) Uwiano wa mali zinazozalisha na jumla ya mali | 78.5% | 68.7% |
| (vi) Ongezeko la amana | 8.8% | 9.3% |
| (vii) Ongezeko la mali | 1.4% | 26.9% |

### Taarifa ya mapato na matumizi kwa mwaka unaoishia 31 Desemba 2019 (kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mwaka wa sasa 31/12/2019 | Mwaka uliyopita 31/12/2018 |
|---|---|---|
| 1. Mapato ya riba | 78,741 | 66,884 |
| 2. Gharama za riba | (20,518) | (18,750) |
| **3. Mapato halisi ya riba (1 kutoa 2)** | **58,223** | **48,135** |
| 4. Madeni viza yaliyofutwa | - | - |
| 5. Punguzo/ongezeko la tengo katika mikopo | (5,874) | (4,253) |
| **6. Mapato yasiyo ya riba** | **41,923** | **45,827** |
| 6.1 Faida /(hasara) zitokanazo na miamala ya fedha za kigeni | 21,031 | 26,032 |
| 6.2 Ada na kamisheni | 20,839 | 19,466 |
| 6.3 Gawio | - | - |
| 6.4 Mapato mengine | 53 | 329 |
| **7. Gharama zisizo za riba** | **(77,125)** | **(75,169)** |
| 7.1 Mishahara na mafao | (42,235) | (38,732) |
| 7.2 Ada na kamisheni | (4,711) | (4,302) |
| 7.3 Gharama nyingine | (30,179) | (32,135) |
| **8. Faida /(hasara) ya uendeshaji** | **17,147** | **14,540** |
| 9. Tengo la Kodi ya mapato | (7,531) | (8,510) |
| **10. Faida /(hasara) halisi baada ya kodi ya mapato** | **9,616** | **6,030** |
| 11. Mapato mengine yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - |
| **12. Jumla ya faida/(hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **9,616** | **6,030** |
| 13. Idadi ya waajiriwa | 484.0 | 506 |
| 14. Mapato kwa hisa | 10.4 | 7.1 |
| 15. Idadi ya matawi | 15.0 | 15.0 |
| **Baadhi ya viashirio vya ufanisi** | | |
| i) Uwiano wa faida kabla ya kodi na wastani wa mali | 1.0% | 0.97% |
| ii) Uwiano wa faida baada ya Kodi na wastani wa fedha za wanahisa | 11.2% | 11.0% |
| iii) Uwiano wa matumizi yasiyo ya riba na mapato ghafi | 75.9% | 79.0% |
| iv) Uwiano wa mapato halisi ya riba na wastani wa mali zinazozalisha | 7.2% | 7.1% |

### Taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia 31 Desemba 2019 (kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mwaka wa sasa 31/12/2019 | Mwaka uliyopita 31/12/2018 |
|---|---|---|
| **I. Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji** | | |
| Mapato/(hasara) halisi | 17,147 | 14,540 |
| **Marekebisho kwa ajili ya** | - | - |
| - Hasara katika mali | 13,198 | 8,327 |
| - Mabadiliko halisi katika mikopo | (12,106) | (120,581) |
| - Faida/hasara kwenye mauzo ya mali | (20) | - |
| - Mabadiliko halisi katika amana | (14,481) | 133,324 |
| - Mabadiliko halisi katika amana za muda mfupi zilizoafikiwa | (25,859) | 29,232 |
| - Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | 41,022 | 17,378 |
| - Mabadiliko halisi katika mali nyingine | (39,527) | (23,921) |
| - Kodi iliyolipwa | (11,240) | (5,171) |
| - Mengineyo (mabadiliko halisi kwenye SMR) | 3,702 | (8,308) |
| **- Fedha halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(28,847)** | **28,831** |
| **II. Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji** | | |
| - Gawio lililopokewa | - | - |
| - Ununuzi wa mali za kudumu | (2,118) | (5,597) |
| - Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | 76 | 238 |
| - Ununuzi wa amana zisizoshughulikiwa na mawakala | (2,000) | - |
| - Mapato kutokana na mauzo ya amana zisizoshughu likiwa na mawakala | - | - |
| - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| **shughuli za uwekezaji** | **(4,043)** | **(5,359)** |
| **III. Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha** | | |
| - Ulipaji wa madeni ya muda mrefu | - | - |
| - Mapato kutokana na utoaji wa madeni ya muda mrefu | 7,000 | - |
| - Mapato kutokana na utoaji wa mtaji wa hisa | 7,162 | 15,000 |
| - Gawio lililolipwa kwa fedha taslimu | - | - |
| - Mabadiliko halisi katika madeni mjengine | - | - |
| - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| **- Fedha halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za kifedha a taslimu mwishoni mwa robo mwaka/mwaka** | **14,162** | **15,000** |
| **IV. Fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslimu** | | |
| **- Ongezeko / punguzo halisi katika fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslimu** | **(18,044)** | **54,461** |
| - Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa robo mwaka/mwaka | 248, 194 | 193,732 |
| **- Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa robo mwaka/mwaka** | **230, 149** | **248, 194** |

| Taarifa ya mabadiliko ya mtaji kwa kipindi kinachoishia 31 Desemba 2019 (kiasi kwa shilingi milioni) | Mtaji wa hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la ziada ya jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa Salio la mwanzo wa mwaka (1-Jan-19)** | 115,270 | 76 | (12,815) | - | 4,559 | 139 | 107,228 |
| Faida / (hasara) halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 9,616 | - | - | - | 9,616 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 217 | 217 |
| Miamala na wanahisa | 7,162 | - | - | - | - | - | 7,162 |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | 4,559 | - | (4,559) | - | - |
| Mengineyo | - | - | (954) | - | - | - | (954) |
| | - | | | | | | |
| **Salio la mwisho wa mwaka (31-Des-19)** | **122,432** | **76** | **405** | **-** | **-** | **355** | **123,269** |
| **Mwaka uliopita salio la mwanzo wa mwaka (1-Jan-18)** | 100,270 | | | | | | |
| Faida / (hasara) halisi baada ya kodi ya mapato | | 76 | (19,866) | 2,329 | 3,250 | (0.1) | 86,060 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | 6,030 | - | - | - | 6,030 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | 139 | 139 |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya lisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | 2,329 | (2,329) | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | (1,308) | - | 1,308 | - | - |
| | 15,000 | - | - | - | - | - | 15,000 |
| **Salio la mwisho wa mwaka (31-Des-18)** | **115,270** | **76** | **(12,815)** | **-** | **4,559** | **139** | **107,228** |

### Baadhi ya maelezo kwa mwaka inayoishia 31 Desemba 2019

Taarifa hizi za fedha ni sehemu ya taarifa ya fedha iliyokaguliwa ya mwaka unaoisha 31 Desemba 2019 ambazo zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya sheria za makampuni Tanzania Cap 212 ya mwaka 2002 na ya sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006. Taarifa hizi za fedha zimekaguliwa na KPMG na kupata hati safi. Taarifa hizi za fedha zimeidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi tarehe 12 March 2020 na kusainiwa na:

| Jina na cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|
| Simon Mponji<br>Mwenyekiti wa Bodi | ........................ | March 12, 2020 |
| Abdi Mohamed<br>Mkurugenzi Mtendaji | ........................ | March 12, 2020 |



Absa Bank Tanzania Limited (yenye usajili namba 38557) inaongozwa na kanuni za Benki Kuu ya Tanzania.
Tarehe 10 Februari 2020 Barclays Bank Tanzania Limited ilibdaili jina kuwa Absa Bank Tanzania Limited.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Zianze jitihada mpya kudhibiti ukosefu ajira

TATIZO la ajira nchini linazidi kushika kasi na kinachoonekana ni uwezo mdogo wa Watanzania hasa wanafunzi wa vyuo vikuu ambao licha ya kuelimika wanashindwa kujianzishia ajira zenye tija ili kumudu maisha yao .

Ni wazi kuwa kinachoonekana ni wengi kutegemea kuajiriwa, baadhi wakizungukia maofisini kila leo kuulizia ajira.

Wakati hayo yakitokea vyuo vikuu, vya kati na ufundi vinatamba kuwa vinaandaa wasomi wanaoweza kujiajiri na kueleza mipango na mikakati iliyopo na juhudi zinazofanyika lakini ukweli ni kwamba havijaweza kutimiza azma hiyo.

Tatizo la ajira linazidi kudhihirika wakati huu ambao vyuo vikuu vinadai kuwa vinawafundisha wanafunzi ujasiriamali na kukabiliana na matatizo ya ukosefu wa ajira, lakini ukweli ni kwamba bado hakujawa na jitihada za kutosha kufanikisha azma hiyo.

Tunaona kuwa ni vyema kubadilisha utaratibu wa kufundisha ili kuangalia jinsi ya kuwaandaa vijana kumudu maisha yao badala ya kuangalia alama za kufaulu kama A na B au ziro.

Tunashauri utaratibu uende mbali kwa kuchambua uwezo wa wanafunzi kuchangia maendeleo yao na ya taifa kwa kuwafundisha ujasiriamali na kujitegemea kunakotokana na rasilimali zinazopatikana kupitia kozi wanazosoma darasani na zile kilichopo katika jamii.

Aidha, rasilimali za Tanzania ambazo ni nyingi zitumike kupunguza tatizo la ajira. Lakini ni kitu gani kinaweza kufanyika kuzitumia ili kuondoa changamoto ya wasomi kushindwa kujitengenezea kazi na pia kukosa wa kuwaajiri?

Vyuo vikuu viwe ' mashamba darasa' mfano Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) kinatoa mafunzo ya kilimo na ufugaji na sayansi za kila aina ikiwamo bayoteknolojia

Tunaona kuwa wakati umefika SUA kutafsiri elimu inayotoa na kubadilisha mifumo ya maisha ya wahitimu wake, majirani wanaokizunguka chuo na hata ukanda wa Morogoro.

Wakati mwingine ni vigumu kufahamu kuwa chuo kinatoa elimu ya kilimo, kwani hakuna hata gereji ya kuchonga bolti za matrekta chuoni,. Kwa hali hiyo wahandisi wa kilimo watawezaje kujiajiri vijijini kama hawawezi hata kuchonga nati na bolti za matrekta ili kufufua kilimo?

Pamoja na kufundisha kilimo ni bora pia kuwa na program zinazoweza kubadili maisha ya wananchi majirani pamoja na wanafunzi wake kwa kuwa na utaalamu mkubwa na elimu ya kilimo ambayo ina mambo mengi.

Mathalani, Watanzania wengi wanahitaji kupata elimu ya kuhifadhi vyakula hasa vijijini. Ni wazi kuwa kama kuna kinachohitajika nchini ni ujenzi wa vihenge vya teknolojia rahisi ili kuhifadhi nafaka, mboga, matunda na bidhaa nyingine za chakula ambazo huoza kutokana na kukosa teknolojia ya kuvihifadhi.

Kinachohitajika ni matumizi ya teknolojia ya kilimo ambayo wanafunzi wanasoma darasani ili yatumike kwenye ujasiriamali na kubadili maisha yao.

Aidha, tunapokitizama Chuo Kikuu cha Ushirika, tunatarajia kiwe kioo cha kuitazama jamii na kuibadilisha kiuwekezaji kwa kuiwezesha kubuni miradi ya uwekezaji, ujasiriamali ubunifu wa biashara inayofanywa na kusimamiwa na chuo hicho ili watu wajifunze zaidi.

Tunaona kuwa ili kumaliza tatizo la ukosefu wa ajira ni lazima ufundishaji utoke nje ya vitabu, mihadhara na alama za kufaulu uende mbele kutafsiri elimu zinazotolewa kwa kuzihusisha na rasilimali zilizopo na kuwafundisha wanafunzi ubunifu wa kuchanganya taaluma na mazingira yanayozunguka na rasilimali zilizopo ili waanzishe na kumudu maisha yao.

Elimu ya juu isaidie wanafunzi kuona jinsi watakavyoweza kujiajiri wakitumia rasilimali kwa mfano bahari, ardhi, madini, mifugo, mazao kama viungo, maua na vivutia watalii ili kuwekeza na kujiajiri badala ya kuendelea kubaki kuwa maskini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kwanini kuhama vyama kuwaletee kuchukiana?

Na Sabato Kasika

MTAZAMO wa baadhi ya watu ni kwamba, mwanasiasa kuhama chama kimoja kwenda kingine ni kosa na wakati mwingine wanamuona kama adui, lakini hilo ni jambo la kawaida katika siasa za Afrika.

Kutokana na mtazamo huo, wapo ambao wamefikia kuchukiana, kwa sababu tu mwenzao amehama, kumbe hilo ni jambo la kawaida kwenye siasa za mfumo wa vyama vingi barani Afrika.

Ni muhimu kuelewa kuwa kuhama chama ni jambo la kawaida katika medani za ushindani wa kisiasa.

Vilevile inawezekana ikawa ni kipimo cha ukomavu wa demokrasia ya kitaifa na watu wake, hivyo wanaohama wasichukuliwe kama maadui, badala yake wanasiasa watambue kuwa hilo ni jambo la kawaida.

Katika siasa kuna sababu kadhaa, ambazo zinamfanya mtu kuhama chama fulani na kujiunga na kingine ikiwamo itikati, sera, utawala, utendaji na hata wakati mwingine uchaguzi wa viongozi.

Katika miaka mitano kuanzia 2015 hadi sasa Watanzania wameshuhudia baadhi ya wanasiasa wakihama kutoka kwenye vyama vya upinzani baada ya kushindwa katika uchaguzi wa ndani wa viongozi.

Wanasiasa hao wamehama kwa sababu za uchaguzi, lakini haina maana kwamba hawahitaji kuaminiwa au wote ni wasaka vyeo, bali inategemea na mazingira ya huko walikotoka.

Wakati mwingine inawezekana kwa sababu ya uhodari wao wa kiuongozi wakatoswa na kuamua kutimiza azma zao za kutumikia jamii, hivyo siyo vibaya wakiomba nafasi za uongozi huko walikohamia.

Mara nyingi wanaohama vyama vyao wakati wa uchaguzi wa ndani huwa ni vigumu kuaminiwa, lakini cha msingi ni kuwasikiliza wakatoa picha halisi ya hali ilivyo kule wanakotoka kama kuna ukweli.

Bahati mbaya wahamaji wamekuwa wakionekana kama maadui kule wanakotoka hata na kule wanakohamia, lakini ukweli ni kwamba ni haki yao ya kidemokrasia kuhama. Mtu kujiunga na chama chochote cha siasa ni hiyari, hakuna sheria inayomlazimisha, bali pale anapotaka kuwania nafasi ya uongozi ndipo linapokuja suala la uanachama.

Kwa hiyo mwanasiasa anapohama kutoka chama kimoja kujiunga na kingine asichukuliwe kama anatengeneza mazingira ya uadui au kutaka kuudhoofisha demokrasia, bali hakuna kinachombana.

Pamoja na hayo, ni vyema pia kuwe na angalizo, kwamba wale wanaohama wasiwe wepesi wa kuponda kule wanakotoka, kwani kufanya hivyo ni kutengeneza uadui usio wa lazima.

Ninasema hivyo, kwa sababu imekuwa ni jambo la kawaida kumsikia mwanasiasa akihama chama na kuanza kutaja hadharani udhaifu wa kule alikotoka hali ambayo sidhani ni ya muhimu.

Dhana ya kuhama chama na kwenda chama kingine ni rahisi hasa kwenye suala la kuvutiwa na sera ikijumuisha tunu, malengo, falsafa, itikadi zake na anapoona katika chama chake hakina huchukua hatua. Lakini, sidhani kama ni sahihi mwanachama kuhama na kuanza 'kushambulia' kule 'alikotoka', hali ambayo wakati mwingine inaweza kuchangia kuleta chuki au uadui miongoni mwa wanasiasa.

Yawezekana wengine wanahama kwa sababu ya kukimbia migogoro, wapo wanapoenda kutafuta nyadhifa waendako au kutafuta maslahi ya kifedha na mambo mengine kwenye siasa.

Kila mmoja ana haki ya kuhama, lakini uamuzi wao usisababishe kuchukiana na hasa kwa kuanza kuponda kule wanakotoka kana kwamba hawawezi kurudi na kumbe mwisho wa siku wanarudi kule walikoponda.

Ikumbukwe kuwa wanachama wa vyama vya siasa wanaweza kupita, lakini mfumo utaendelea kuwapo kama kawaida, hivyo ingawa mtu kuhama chama ni hiyari, lakini pia wahamaji wanatakiwa kutafakari.

Ushauri ni kwamba, wasiwe wepesi wa 'kushambulia au kuponda' kule wanakotoka, watambue kuwa siasa ni mzunguko, kwani leo wanaweza kuwa katika chama fulani kisha wakahama halafu baadaye wakarudi tena.

# TANGAZO

# Bank of India (Tanzania) Ltd.

*Relationships beyond banking*

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)**

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA KWA UMMA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2019

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | | Mwaka wa sasa 31-DES-19 | Mwaka Uliopita 31-DES-18 |
|---|---|---|---|---|
| A. | | **MALI** | | |
| | 1 | Fedha Taslimu | 722 | 849 |
| | 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 15,414 | 11,585 |
| | 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 46,997 | 49,487 |
| | 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 3,357 | 16,109 |
| | 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| | 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| | 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| | 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| | 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 7,318 | 4,737 |
| | 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| | 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 69,247 | 69,993 |
| | 12 | Mali Nyingine | 3,861 | 1,905 |
| | 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| | 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| | 15 | Kodi iliyoahirishwa | 449 | 299 |
| | 16 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 744 | 1,267 |
| | **17** | **JUMLA YA MALI** | **148,109** | **156,230** |
| B. | | **B. DHIMA** | | |
| | 18 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 41,018 | 50,067 |
| | 19 | Amana za Wateja | 66,140 | 68,764 |
| | 20 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | 21 | Amana Maalumu | - | 22 |
| | 22 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 39 | - |
| | 23 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 25 | 44 |
| | 24 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 3,090 | 2,224 |
| | 25 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| | 26 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| | 27 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| | 28 | Dhima Nyingine | 2,419 | 905 |
| | **30** | **JUMLA YA DHIMA** | **112,732** | **122,028** |
| | **31** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **35,377** | **34,203** |
| C. | | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| | 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,500 | 21,500 |
| | 32 | Akiba ya Mtaji | 3,876 | 3,341 |
| | 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 7,824 | 6,123 |
| | 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 2,177 | 2,484 |
| | 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | 755 |
| | 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| | **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **35,377** | **34,203** |
| | 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 11,026 | 5,978 |
| | 39 | Mikopo Chechefu | 6,123 | 4,967 |
| | 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 1,938 | 1,361 |
| | 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D. | | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| | (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 23.89% | 21.89% |
| | (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 8.60% | 6.96% |
| | (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 66.43% | 60.04% |
| | (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali | 46.75% | 44.80% |
| | (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 83.43% | 79.51% |
| | (vi) | Ongezeko la Amana | -9.82% | -12.70% |
| | (vii) | Ongezeko la Mali | -5.20% | -10.38% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOSHIA 31 DESEMBA 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mwaka wa sasa 31 Des 2019 | Mwaka Uliopita 31 Des 2018 |
|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 12,135 | 13,547 |
| 2 Gharama za Riba | (4,989) | (5,488) |
| 3 **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **7,146** | **8,059** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | 2 | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (710) | (945) |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **962** | **1,077** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 223 | 234 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 738 | 839 |
| 6.3 Gawio | - | 3 |
| 6.4 Mapato Mengine | - | - |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | **(4,449)** | **(4,541)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (2,300) | (1,540) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | (172) | (172) |
| 7.3 Gharama Nyingine | (1,977) | (2,830) |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **2,951** | **3,649** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | (774) | (1,165) |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **2,177** | **2,484** |
| 11 **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa robo ya mwaka /mwaka** | **2,177** | **2,484** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 29 | 29 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 101 | 116 |
| 15 Idadi ya Matawi | 2 | 2 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.94% | 2.21% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 6.26% | 7.25% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 33.97% | 31.05% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 5.69% | 5.57% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa sasa 31 Des 2019 | Mwaka uliopita 31 Des 2018 |
|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 2,951 | 3,649 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | |
| | - Hasara Katika Mali nyinginezo | - | 36 |
| | - Hasara na Kuchakaa Katika Mali | 333 | 224 |
| | - Mikopo iliyofutwa na Tengo la mikopo | (709) | (2,151) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | (3) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (11,673) | (17,145) |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 892 | 4,237 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (2,845) | (4,743) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 495 | (467) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (2) | 845 |
| | -Mabadiliko Halisi mikopo ya muda mrefu itolewayo na mabenki mengine | (6,864) | 2,676 |
| | - Kodi Iliyolipwa | (810) | (1,625) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | ***(18,233)*** | ***(14,467)*** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (90) | (989) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | (29) |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | 5 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | ***(90)*** | ***(1,014)*** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | (430) | (645) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | ***(430)*** | ***(645)*** |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| | **Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | **(18,753)** | **(16,126)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka / Mwaka | 42,185 | 58,311 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka / Mwaka** | **23,432** | **42,185** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo Juu ya bei ya Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2019** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2019** | 21,500 | - | 8,607 | 3,341 | 755 | - | **34,203** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 2,177 | - | - | - | **2,177** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (387) | - | - | - | **(387)** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (1,174) | 1,174 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 755 | - | (755) | - | - |
| Mengineyo (mikopo iliyofutwa) | - | - | 22 | (638) | - | - | **(616)** |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2019** | **21,500** | **-** | **10,001** | **3,876** | **-** | **-** | **35,377** |
| **Mwaka uliopita 2018** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2018** | **21,500** | **-** | **8,496** | **3,215** | **1,088** | **-** | **34,299** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 2,484 | - | - | - | **2,484** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (430) | - | - | - | **(430)** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (1,943) | 2,277 | (333) | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | (2,151) | - | - | **(2,151)** |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2018** | **21,500** | **-** | **8,607** | **3,341** | **755** | **-** | **34,203** |

**BANK OF INDIA (TANZANIA) LTD**
**DAR ES SALAAM**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Mr. Ashwani Kumar Negi<br>Mkurugenzi Mtendaji | Imesainiwa | 31.03.2020 |
| Mr. Heriabdiel Ayoh<br>Mkuu wa Fedha | Imesainiwa | 31.03.2020 |
| Mr. Allen Richard<br>Mkaguzi Mkuu wa Ndani | Imesainiwa | 31.03.2020 |

Hapo juu ni baadhi ya taarifa kutoka katika ukaguzi wa taarifa ya fedha ya benki kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba 2019, na zimeandaliwa kwa kulingana na sera za kimataifa (IFRS). Taarifa hizi za fedha zimekaguliwa na mkaguzi aliyeidhinishwa Baker Tilly DGP & CO na zimepata hati safi.

Taarifa hii ya fedha imepitishwa na Bodi ya Wakurugenzi na imesainiwa na wakurugenzi wafuatao kwa niaba ya wenzao

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| 1. Dr. Benard E. Mnzava- Mkurugenzi | Imesainiwa | 31.03.2020 |
| 2. Mr. S.K Mukherjee - Mkurugenzi | Imesainiwa | 31.03.2020 |

# PM: Shule, vyuo kuendelea kufungwa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema agizo la kufungwa kwa shule za awali, msingi, sekondari na vyuo vyote vya elimu ya kati na vya elimu ya juu litaendelea kubaki vile vile hadi hapo serikali itakapotoa tamko jingine.

Pia, Waziri Mkuu amesema Rais Dk. John Magufuli, amesitisha maadhimisho ya Sherehe za Muungano (Aprili 26) pamoja na Sikukuu ya Wafanyakazi (Mei Mosi) ili kuepuka msongamano na kuendelea kuzuia virusi vya corona visisambae zaidi.

Waziri Mkuu ameyasema hayo jana, katika kikao cha Kamati ya Kitaifa ya Uratibu wa Mapambano dhidi ya ugonjwa wa homa ya mapafu unaotokana na maambukizi ya virusi vya corona (Covid-19).

Alisema hadi jana, nchini kuna jumla ya watu 53 waliobainika kuwa na virusi vya corona ikiwa ni ongezeko la wagonjwa wanne ambao wote wapo jijini Dar es Salaam.

Amesema serikali bado haijatangaza kuhusu kufunguliwa kwa shule, vyuo na shughuli za michezo pamoja na misongamano isiyokuwa ya lazima, hivyo maeneo hayo yataendelea kusalia katika karantini na wanafunzi wote wandelee kubakia majumbani kwao.

Hata hivyo, Waziri Mkuu amesema Rais Dk. Magufuli ameagiza Sh. milioni 500 ambazo zilitengwa kwa ajili ya maadhimisho ya miaka 56 ya Sherehe za Muungano zipelekwe kwenye mfuko wa kupambana na Covid-19 wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Pia, Waziri Mkuu amewaomba wadau mbalimbali waendelee kuiunga mkono serikali katika mapambano dhidi ya virusi vya corona kwa kuwa janga hilo ni kubwa na wanaweza kutuma fedha kupitia akaunti Na: 9921159801 yenye jina la National Relief Fund Electronic.

Kadhalika, Waziri Mkuu amesema elimu ya tahadhari ni muhimu ikaendelea kutolewa kwa wananchi ili waweze kujikinga na maambukizi ya homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona. "Kama si lazima kutoka, wananchi waendelee kutulia majumbani mwao."

Amesema wakuu wa mikoa na wilaya waendelee kusimamia utoaji wa elimu ya kujikinga na virusi hivyo hasa katika Mkoa wa Dar es Salaam ambao unaongoza kwa kuwa na wagonjwa wengi ikifuatiwa na Zanzibar.

"Ni muhimu wananchi wake wakapewa tahadhari ya namna ya kijikinga."

Ameagiza wataalamu wanaosimamia utoaji wa huduma katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya watu wenye maambukizi ya corona wakiwamo madaktari wote wapewe vifaa vya kijikinga ili kuhakikisha hawapati maambukizi ya ugonjwa huo.

Amesema watu waliokutana na wagonjwa waendelee kufuatiliwa kwa umakini na wahusika wawashirikishe viongozi wote hadi wa ngazi za chini na kwamba athari za kiuchumi zinazojitokeza kufuatia ugonjwa huo ziendelee kuchambuliwa.

Machi 17, 2020 na Machi 18, 2020, serikali ilitangaza kuzifunga shule za awali, msingi, sekondari na vyuo vyote vya elimu ya kati na vya elimu ya juu kwa muda wa siku 30 na kwamba wanafunzi wa kidato cha sita waliopaswa kuanza mitihani Mei 4, 2020, nao wangepaswa kusubiri wizara ifanye utaratibu mwingine kulingana na matokeo ya hali ya maambukizi.

Akitangaza uamuzi huo, Waziri Mkuu pia alisisitiza kuwa mikusanyiko yote mikubwa ya ndani na nje isiyo ya lazima imesitishwa ikiwamo shughuli za michezo, matamasha ya muziki, mikutano mbalimbali ikiwamo ya shughuli za kisiasa, mahafali na shughuli nyingine za kijamii.

NHC
SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA
TUNAJENGA TAIFA LETU

## SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA
## TAARIFA KWA UMMA

Shirika la Nyumba la Taifa, linapenda kuwatangazia wateja wake wote na umma kwa ujumla kuwa linaendelea kuwapatia huduma zake kama kawaida. Hata hivyo, ili kuepuka msongamano katika kipindi hiki cha Corona (COVID 19) na kwa kuzingatia maelekezo ya Serikali yetu ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huu, tunawashauri wateja wetu kutumia zaidi mawasiliano ya simu na mtandao kupata au kulipia huduma zetu.

Hatua hii itaepusha msongamano wa wateja wetu na kurahisisha kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona.

Kwa malipo ya ankara yako ya kodi ya nyumba tumia mfumo wa malipo wa Serikali (GePG) ambao ni rahisi na salama. Unaweza pia kulipia kwa njia ya Benki, Mawakala wetu na simu yako ya mkononi.

**Kwa maelezo zaidi, wasiliana nasi kupitia:-**

**Simu: +255 784 105 200 na +255 222 162 800 / +255 222 105 002/3/4**

Baruapepe: dg@nhc.co.tz
Imetolewa na Kitengo cha Mawasiliano kwa
Umma na Huduma kwa Jamii, Shirika la Nyumba la Taifa

## NOTISI/TANGAZO LA MNADA

Kwa idhini tuliyopewa na AKIBA **COMMERCIAL BANK PLC, MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD** tunatangaza kuuza dhamana za wadaiwa sugu walioshindwa kulipa mikopo yao katika Benki tajwa hapo juu kama watashindwa kulipa madeni yao ndani ya siku ISHIRINI NA NANE (28) tangu kutolewa kwa tangazo hili. Minada hii itafanyika kama inavyoonesha hapa chini kwenye jedwali;

| S/N | JINA LA MTEJA | TAWI LA MDAIWA | UMILIKI WA DHAMANA | AINA YA DHAMANA NA MAHALI ILIKO | TAREHE NA MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 001 | EASTER WILLIUM NJIU | KARIAKOO | EASTER WILLIUM NJIU | KIWANJA KILICHOENDELEZWA BUNJU CHENYE HATI NAMBA 68435, KITALU 26, BLOCK 8 | 13/05/2020 SAA 04.00 |
| 002 | BASHIRU ISSA JUMA | ILALA | BASHIRU ISSA JUMA | NYUMBA AMBAYO HAIJAKAMILIKA PUGU MWAKANGA YENYE LESENI NO.139476 | 14/05/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 003 | JUMA NURU MUSHI | TEMEKE | JUMA NURU MUSHI | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI KIJICHI KARIBU NA SHULE YA MSINGI KIJICHI MBAGALA KUU | 21/05/2020 SAA 04.00 MCHANA |
| 004 | MWANAHAMISI ATHUMAN LUMAJA | MBGALA | ELVIS ERICK LUYEGO | NYUMBA AMBAYO HAIJAKAMILIKA VIKINDU VIANZ YENYEMKATABA WA MAUZIANO | 22/05/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 005 | MARIAM MOHAMED LIKWAYU | MBAGALA | MR/MRS CHEMBERA | NYUMBA AMBAYO HAIJAKAMILIKA VIKINDU VIANZI YENYE MKATABA WA MAUZIANO | 22/05/2020 SAA 08:00 MCHANA |
| 006 | IDRISA HAMIS SHABANI | KARIAKOO | IDRISA HAMISI SHABANI | NYUMBA AMBAYO HAIJAKAMILIKA YENYE HATI YA MAUZIANO YA MAUZIANO ILIYOKO MBAGALA MZINGA | 25/05/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |

**Masharti ya mnada**
1. Dhamana itauzwa kama ilivyo na mahali iliko.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku hiyo hiyo ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote, kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona, kukaguwa, kuhamisha umiliki, na zingine zinazoambatana na hili ni juu ya mnunuzi.

**KWA TAARIFA ZAID WASILIANA NA:**
**AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, AU Maseto Auctioneer,**
**MKURUGENZI MTENDAJI, MKURUGENZI MTENDAJI,**
**P.O BOX 669, P.O BOX 75087,**
**DAR ES SALAAM DAR ES SALA**
**Tel+255 02221183403 +255 765 999 000 AU +255 787 288 442 AU +255 762 260 787**

## NOTISI/TANGAZO LA MNADA

Kwa idhini tuliyopewa na **AFRICAN BANKING CORPORATION TANZANIA LIMITED (BancABC) MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD** tunatoa notisi ya siku ishirini na nane kwa wadaiwa walio orodheshwa kwenye tangazo hili kulipa madeni yao yote wanayodaiwa. Kama watashindwa kulipa madeni yao ndani ya muda wa siku 28 tangu kutolewa kwa tangazo hili. Basi tutaendesha Minada ya hadhara ya kunadi mali hizo na minada hiyo itafanyika mahali na wakati kama jedwali inavyoonesha;

| S/N | JINA LA MTEJA | UMILIKI WA DHAMANA | AINA YA DHAMANA NA MAHALI ILIKO | TAREHE NA MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 001 | INTER 33 34 LIMITED | RICHARD KARUMUNA RWEYONGEZA | SHAMBA NO. 2019, HATI MILIKI NO. 52398, ECARI 224 LILOKO DISUNYARA (MLANDIZI) - WILAYA YA KIBAHA | 16/05/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 002 | CORNER BAKERY AND CONFECTIONARY LTD | THE CHEF LIMITED | VIWANJA TOFAUTI VIPO SEHEMU MOJA KIBUGUMO KIGAMBONI VYENYE HATI NO. 1081, 1082,1083,1084,1085 L.O | 19/05/2020 SAA: 04:00 ASUBUHI |
| 003 | PAULA INTERBUSINESS CO. LTD | ABDUL SAMAD HASSAN T/A PAULA INTERBUSINESS CO. LTD | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOKO ENEO LA MAGOGONI KIWANJA NO. 1178, HATI MILIKI NO. 80179 KITALU 'F' | 19/05/2020 SAA: 08:00 MCHANA |

**Masharti ya mnada**
1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku hiyo hiyo ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kutoka siku ya mnada ili kukamilisha malipo yote, ukishindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona, kukaguwa, kuhamisha umiliki, na zingine zinazoambatana na hili ni juu ya mnunuzi.

**KWA TAARIFA ZAID WASILIANA NA:**
**BANKABC TANZANIA LIMITED, AU Maseto Auctioneer,**
**MKURUGENZI MTENDAJI, MKURUGENZI MTENDAJI,**
**P.O BOX 31, P.O BOX 75087,**
**DAR ES SALAAM DAR ES SALAAM**
**Tel+255 222119422 - 3 +255 787 288 442 AU +255 765 999 000**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 15/03/2019

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya ALHAMISI tarehe 16/04/2020 kampuni ya **ESTIM CONSTRUTION CO. LTD** itasafirisha Mzigo Motor Grader wenye vipimo vikubwa. Kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **VIGWAZA** kupitia **CHALINZE NA MSATA** Gari hilo yana namba za usajili:
   **T235 CHW/ T 106 AYZ**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   Urefu - mita 20.00
   Upana - mita 3.0
   Kimo - mita 4.8

3. Njia itakayotumika: **DAR ES SALAAM** hadi VIGWAZA kupitia **CHALINZE NA MSATA**
   Gari litasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

# Watakiwa mtandao kulipia gharama kujikinga corona

**Na Felix Andrew**

WATEJA wote wanaohitaji kusajili sehemu za biashara au bidhaa za chakula na dawa, watalazimika kufanya hivyo kwa njia ya mtandao unaojulikana kwa lugha ya kigeni kama Online Application System (OAS), Shirika la Viwango Tanzania (TBS) limesema.

Meneja wa Tehama wa TBS, Jabir Saleh Abdi, alisema kwa sasa maombi ya shughuli za kukagua mizigo yanafanyika mtandaoni

Alisema usajili wa majengo, bidhaa kama za chakula na dawa ambazo awali zilikuwa zinafanywa na iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), kwa sasa zinafanywa na TBS kwa njia ya mtandao kuanzia Julai Mosi, 2019.

"Tumeamua kuendeleza mfumo huu wa maombi kupitia mtandao ili kuwawezesha wafanyabiashara kusajili majengo, dawa au kupata vyeti vitakavyowawezesha kufanya biashara zao kihalali," alisema.

Abdi anasema TBS imeamua kuwasaidia wafanyabiashara kutimiza ndoto ya mapinduzi ya viwanda iliyoanzishwa na Rais John Magufuli miaka kadhaa iliyopita.

Mbali na kusajili maombi ya eneo au bidhaa mtandaoni, wafanyabiashara wanaweza kupokea taarifa za fedha au vyeti au kibali bila kulazimika kwenda ofisi za TBS.

Alisema pia OAS, inawawezesha wateja wa shirika hilo kutuma mtandaoni maombi ya huduma nyingine kama ukaguzi wa bidhaa nchini, ukaguzi wa bidhaa kabla ya kuingia nchini na huduma ya kutoa mizigo bandarini.

Alisema chini ya mfumo wa ukaguzi wa bidhaa nchini , mteja anaweza kukubali au kukataa taarifa ya ukaguzi kupitia mtandaoni.

Meneja huyo alisema maombi ya huduma ya kutoa mizigo bandarini yanapatikana pia mtandaoni, na yanasaidia mteja kukaguliwa bidhaa zake bandarini au mpakani kwa lengo la kupunguza gharama za utunzaji.

"AOS inasadia wateja kuepuka virusi vya corona, kwani atafanya maombi yote kwa njia ya mtandao, bila kulazimika kutoka nje ya ofisi au nyumbani na kukutana na watu wengi kitu ambacho ni hatari kwa kipindi hiki," aliongeza.

Alisema tangu usajili kwa njia ya mtandao ulipoanza mwaka mmoja uliopita, kumekuwa na mwitikio mzuri kutoka kwa wafanyabiashara.

Akitolea mfano anasema kuwa wamepokea maombi mtandaoni 4,200 ya kusajili majengo, bidhaa aina za vyakula na dawa.

Kwa mujibu wa meneja huyo, TBS pia imepokea jumla ya maombi 89,072 kwa njia ya mtandao kutoka kwa mawakala wa kutoa mizigo bandarini wa kipindi hicho.

Aidha, alisema OAS imezuia viashiria vya rushwa vinavyoweza kutokea endapo ingefanyika kwa njia ya kuonana.

Anaongeza kuwa kwa sasa hakuna mlundikano wa mafaili na muda wa kuhudumiwa mteja umepungua hadi siku tatu au chini ya hapo.

Kadhalika, alisema imepunguza sana matumizi ya karatasi, hivyo kupunguza gharama kwa shirika na wateja.

Anasema mfumo huo umepunguza pia gharama za mawasiliano, vifaa vya kiofisi na gharama za usafiri kwa wateja ambao awali walilazimika kwenda ofisini kwao.

Pia mfumo huu uko wazi kwani unawezesha mteja kujua hali ya maombi yake mtandaoni bila kulazimika kumuuliza mhusika wa shirika

Kuhusu changamoto , alisema awali ilikuwa ni baadhi ya wateja ambao walikuwa hawana uelewa wa kutosha kutumia mfumo huo.

"Tuliendesha kampeni ya namna ya kutumia mfumo huu, na sasa wengi wao wanauelewa na kuutumia."

Kuhusu wadukuzi, alisema hawana tatizo kwani mfumo huo unalindwa vizuri.

"Mfumo wetu uko huru kutoka kwa wadukuzi, tunashirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao (eGA) kuhakikisha kuwa hakuna changamoto yoyote inayoweza kutokea.




Mhifadhi Utalii wa Hifadhi ya Milima ya Udzungwa, Richard Hayri (kulia), akitoa elimu ya uhifadhi na utalii wa ndani, kwenye msitu wenye mizinga, kwa baadhi ya wajumbe wa kikundi cha ufugaji bora nyuki cha "Usia wa Baba", kinachopakana na hifadhi hiyo, katika kijiji cha Msufuni, Kata ya Mkula, Tarafa ya Mang'ula, wilayani Kilombero, mkoani Morogoro juzi. Katikati ya Mhifadhi ni Mwenyekiti wa kikundi hicho, Daniel Hollow na Mjumbe Richard Malipa. Kikundi hicho, kinachofadhiliwa na hifadhi hiyo, na Mfuko wa Uhifadhi wa Milima ya Tao Mashariki (EAMCEF), kina mizinga ya kisasa 120, huvuna kiasi cha lita 600 kwa msimu mzuri. **PICHA: DANIEL SABUNI**

## Katavi yatoa fursa kwa Tari uzalishaji mbegu za kisasa

**Na Ashton Balaigwa,** KATAVI

MKUU wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera, ameahidi kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari), ili kutumia teknolojia zake za kisasa za mazao mbalimbali ili yaweze kuzalishwa katika mkoa huo.

Mazao hayo yale yanahitajika kutumika kama malighafi katika uchumi wa viwanda.

Homera alitoa ahadi hiyo wakati akizungumza na Mkurugenzi Mkuu wa Tari, Dk. Geofrey Mkamilo, aliyemtembelea mkoani humo kuweka mikakati ya uzalishaji wa mazao ya chakula na ya kimkakati ikiwamo zao la michikichi, korosho, ufuta, alizeti na karanga kwa lengo la kusaidia uchumi wa viwanda.

Homera alisema wameshaanza mikakati ya uzalishaji wa mazao hayo katika wilaya zote ili kufanya mkoa huo kuwa na uhakika na usalama wa chakula pamoja na ziada.

Naye Dk. Mkamilo alisema wameshafanya utafiti wa mbegu za mazao mbalimbali ya teknolojia ya kisasa yakiwamo yanayohimili ukame na changamoto za wadudu, ambayo yameonyesha kuongeza uzalishaji wa chakula nchini.

Alisema Tari imepewa jukumu la kuratibu zao la michikichi nchini ikiwamo kuzalisha mbegu zake na kuzigawa bure kwa wakulima.

Homera alimuahidi Mkurugenzi huyo wa Tari kuwa, wapo tayari kuwapatia eneo katika mkoa huo lenye ukubwa wowote kwa ajili kufanyika utafiti na ujenzi wa ofisi zake, na kuwataka kuwasilisha ombi hilo kwa kufuata taratibu.

# Mil. 218/- kumaliza kero ya stendi Kahama

**Na Ndalike Sonda,** KAHAMA

SIKU chache baada ya wafanyakazi na abiria katika stendi ndogo ya Cdt mjini Kahama mkoani Siyinyanga, kulalamikia ubovu wa miundombinu ya stendi hiyo, Serikali imesema Sh. milioni 218 zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa stendi hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, alisema fedha hizo zimetengwa kupitia Halmashuri ya Mji wa Kahama, na kwamba kitachukua siku 30 ili kukamilisha ukarabati huo.

Macha alisema eneo hilo asili yake lilikuwa na mkondo wa maji na ardhi yake inahifadhi maji, hivyo ni lazima wachimbe ardhi yote yenye maji ili kuboresha ujenzi huo, na kwamba magari yote yatahamia katika stendi ndogo iliyopo Kata ya Majengo mjini Kahama. Alisema ujenzi huo unategemea kuanza muda wowote na kuwa wanasubiri magari ya stendi ya Cdt yahame.

Alisema kwamba, vibarua wote watakaofanya kazi watatoka eneo hilo, na kwamba barabara zote za kuingia na kutoka katika standi hiyo zitaboreshwa. "Stendi hiyo tunaiboresha kwa kiasi cha Sh. milioni 218 na utachukua siku 30, tunawaomba watu wa stendi wahame kwa muda ili kazi ianze,' alisema. Diwani wa Kata ya Kahama Mjini, Hamidu Juma, alipongeza serikali kwa kutenga bajeti hiyo, na kuwataka wafanyakazi kukubali kuhama bila msukumo ili kupisha ukarabati huo kwa lengo la kuboresha stendi ya Cdt.

Slyvester Opata, mwenyekiti wa stendi ya Cdt, alisema wafanyakazi wa stendi hiyo hawakubaliani na agizo la serikali la kuhamia stendi ya Majengo badala yake wahamie stendi kuu ya mabasi mjini Kahama au Stendi hiyo itengenezwe kwa awamu mbili ili kuruhusu mabasi kuendelea kufanya kazi katika stendi hiyo badala ya kuhama.

Stendi ya Cdt imeharibika kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha, hali iliyosababisha baadhi ya magari na abiria kuzama kutokana na uwapo wa mashimo na ardhi kutitia.

# Mgodi walipa NSSF bil 5/- michago ya wafanyakazi 2,038 Januari, 2020

JUMLA ya Sh. bilioni 5.01 zimelipwa na Mgodi wa madini ya dhahabu wa Geita (GGM), mwezi Februari, 2020 kwa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), ikiwa ni mchango wa mwezi Januari 2020 kwa wafanyakazi 2,038.

Aidha, katika mwezi huo, wanachama 6,128 ambao wameajiriwa na makandarasi 39 wanaotoa huduma ndani ya mgodi huo walikuwa wameandikishwa na NSSF na kuchangiwa wastani wa Sh. bilioni 1.3.

Majibu hayo yalitolewa jana bungeni na Ofisi ya Waziri Mkuu katika swali lililoulizwa na Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Upendo Peneza (pichani).

Katika swali lake, Peneza alisema kampuni ambazo zinafanya kazi ndani ya mgodi huo zimekuwa zikilalamikiwa na wananchi wanaofanya kazi kwa kutopeleka fedha kwenye mifuko ya jamii na kutowapa mikataba. "Je, Serikali inachukua hatua gani kukomesha malalamiko hayo?" alihoji.

Kwa majibu wa majibu ya ofisi hiyo, watumishi wanaofanya kazi katika mgodi huo wamegawanyika katika makundi mawili, ambayo ni wale walioajiriwa moja kwa moja na GGM na wale walioajiriwa na makandarasi wanaotoa huduma ndani ya mgodi huo.

Ilisema kwa Februari Sh. bilioni 5.01 zililipwa na GGM kwa watumishi 2,038 walioajiriwa moja kwa moja na GGM huku Sh.Bilioni 1.3 zikilipa michango kwa wanachama 6,128 ambao wameajiriwa na makandarasi 39.

Hata hivyo, Ofisi hiyo ilisema imekuwa ikifanya ukaguzi katika maeneo mbalimbali ya kazi ikiwamo ya migodini kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa sheria za kazi.

"Kupitia Ofisi ya Kazi ya Mkoa wa Geita, ukaguzi katika mgodi wa GGM ikiwamo kandarasi zinazofanya kazi chini ya kampuni hiyo umekuwa ukifanyika ili kulinda haki na maslahi ya wafanyakazi katika maeneo hayo," ilisema.


Aidha, ilisema katika kipindi cha mwaka 2019/20, ukaguzi umefanyika katika Kampuni za GGM, Africa Underground Mining Services, Capital Drilling, GHP Transportaton, Security Group Africa, Fabec Construction, GIPCO Construction, East Africa Radiators, Paulando Enterprises, AVLOW (T) Ltd na EPSON Ltd.

"Aidha, baada ya ukaguzi huo hatua stahiki kwa mujibu wa sheria zimechukuliwa ikiwamo kuwapatia Amri Tekelezi waajiri waliobainika kukiuka sheria za kazi na baadhi ya wafanyakazi raia wa kigeni kufutiwa vibali vyao vya kazi," ilisema.

Ilisisitiza kuwa, itaendelea kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kuhakikisha maelekezo yanayotolewa yanazingatiwa ipasavyo, hivyo kumarisha uhusiano mwema kati ya waajiri na wafanyakazi kwenye maeneo hayo.



# Suma JKT kuagiza nje matrekta 100 kabla Juni




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa, Shirika la Uzalishaji Mali katika Jeshi la Kujenga Taifa (Suma JKT), linatarajia kuagiza matrekta mengine 100 na zana zake kabla ya mwezi Juni, 2020. Mpango huo ulitangazwa bungeni jana na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, katika swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Martha Mlata. (pichani)



Katika swali lake, Mlata alihoji ni sababu zipi zilisababisha Suma JKT kutoendelea na mradi wake wa matrekta.

Katika majibu ya Wizara hiyo, Suma JKT inaendelea na mradi wake wa matrekta kwa kununua matrekta, vipuri na zana zake na kuuza katika awamu tofauti tofauti.

Ilisema katika mwaka wa fedha 2018/19 mradi uliagiza matrekta 100 na kufanikiwa kuuza matrekta 67.

"Pia Suma JKT inatarajia kuagiza matrekta mengine 100 na zana zake kabla ya Juni, 2020," ilisema.

Hata hivyo, ilisema kutokana na kasi ndogo ya ulipaji madeni ya matrekta, mradi sasa unaagiza na kuuza matrekta kwa fedha taslimu na kwa bei nafuu ili kumfanya mkulima kumudu kununua.

"Shirika linaendelea kufuatilia madeni ya matrekta na mradi unaendelea kufanya biashara ya kuagiza na kuuza matrekta," ilisema.

# 'Wazo uanzishaji bodi zabibu bado'

WIZARA ya Kilimo imesema kwa sasa haina mpango wa kuanzisha bodi ya zabibu na badala yake ipo kwenye hatua za awali za mapendekezo ya kuanzishwa kwa mamlaka ya mazao ya bustani.

Hayo yalielezwa bungeni jana, katika majibu ya Wizara hiyo kwenye swali la Mbunge wa Chilonwa (CCM), Joel Makanyaga (pichani chini).

Katika swali lake, Makanyaga alisema Dodoma kwa kiasi kikubwa na muda mrefu imekuwa ikitegemea sana zabibu kama zao la biashara.

Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wataalamu wa kilimo hicho wanapatikana ili kuwasaidia wakulima.

"Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha bodi ya zabibu ili kukuza kilimo cha zabibu?" alihoji.

Katika majibu ya Wizara hiyo, ilisema kwa kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI -Makutupora) ina jukumu la kuzalisha na kusambaza teknolojia bora za kilimo cha zabibu, ikiwamo kuhakikisha wataalamu katika mkoa huo na maeneo mengine nchini wanajengewa uwezo ili kuwasaidia wakulima.

Aidha, ilisema katika mwaka 2019 kwa kushirikiana na wadau wengine kama Kilimo Endelevu Tanzania na Faida Mali imefanikiwa kusambaza teknolojia bora za zabibu kwa wakulima na wadau mbalimbali 3,065 katika kata za Chihanga na Makutupora.

"Ili kuongeza utaalamu kwa watafiti wa TARI-Makutupora kuhusiana na taaluma ya mizabibu, Taasisi hiyo imeendelea kuwawezesha wataalamu wake kupata mafunzo ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu kwenye nchi zilizobobea katika kilimo cha mizabibu kama vile Afrika Kusini na Ujerumani,"ilisema.

Hata hivyo, ilisema utaalam na uzoefu utakaopatikana utafikishwa kwa wagani na wakulima wa mfano ili kuzalisha zao hilo kwa tija na kulingana na vigezo vya masoko.

Kuhusu bodi, ilisema inatambua umuhimu wa chombo au taasisi ambayo ingefaa kusimamia kwa karibu uendelezaji wa zao la zabibu, hata hivyo kwa sasa haina mpango wa kuanzisha bodi na badala yake ipo kwenye hatua za awali za mapendekezo ya kuanzishwa kwa mamlaka ya mazao ya bustani.

"Aidha, zao la zabibu litakuwa ni mojawapo ya mazao yatakayoendelezwa chini ya usimamizi wa mamlaka hiyo," ilisema.

Kadhalika, ilifafanua kuwa imeendelea kuweka mikakati ya kusimamia na kuendeleza zao hilo kufikia mwaka 2024/25 ikiwamo kuongeza upatikanaji wa masoko kutoka asilimia 65 hadi 85, kuongeza tija ya uzalishaji kutoka tani 6.25 kwa hekta hadi tani 20 kwa hekta.

Pia ilisema kuimarisha uwezo wa TARI Makutupora kuzalisha miche bora kutoka miche 100,000 kwa msimu hadi miche 300,000 kwa msimu, kuweka mazingira bora ya uwekezaji katika tasnia ya zabibu pamoja na kutenga na kulinda ardhi kwa ajili ya kilimo hicho.



# Mwaka mmoja mapinduzi Sudan, hali bado ni tete

Ukurasa 13





siasa

JUMATANO APRILI 15, 2020

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

Ukurasa 14

## Aliyoasisi Sokoine miaka 36, fikra zimebaki palepale

**Na Sabato Kasika**

CHAMA cha Tanzania Labour Party (TLP), kinatarajia kupitisha jina la Rais John Magufuli, kuwania nafasi ya urais kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka huu, kwa vile TLP haina mpango wa kutangaza mgombea anayepingana na Rais.

Huo ni uamuzi utakaofikiwa na Mkutano Mkuu utakaofanyika Mei 9 mwaka huu jijini Dar es Salaam ikiwa ni mwendelezo ulioanzishwa na vikao vya halmashauri kuu ya chama tangu Mei mwaka jana. Ndivyo, Mwenyekiti wa TLP, Augustino Mrema, anavyosema katika mazungumzo yake na gazeti hili wiki hii, kuelezea kile kinachoendelea kwa sasa ndani ya TLP.

"Mkutano mkuu ndicho kikao kikubwa cha chama, baada ya vikao vyote vya chini na sasa tutakutana na kumpitisha rasmi mgombea huyo wa CCM, ili kuwania nafasi ya urais na kumalizia miaka yake mitano iliyobakia," anasema Mrema.

Anaeleza kuwa TLP itajikita zaidi kwenye nafasi za ubunge na udiwani na kumwachia urais, mgombea wa CCM na kwamba hayo ni miongoni mwa maamuzi watakayofikia watakapokutana mwezi ujao.

"Mchakato wa kumpitisha Magufuli ulianza tangu Mei mwaka jana katika vikao vya Halmashauri Kuu ya Taifa, bado tunaendelea na tukitarajia kuhitimisha uamuzi huu muhimu Mei 9," anasema.

**ANATAJA SABABU**

Kiongozi huyo wa chama cha upinzani anataja sababu kadhaa za chama chake kufikia uamuzi huo ikiwamo kukosa mgombea mwenye kiwango cha utendaji kama cha Rais Magufuli.

"Hatuna mgombea wa kiwango cha Magufuli, na si kwetu tu bali vyama vyote vya upinzani havina mgombea wa aina hiyo, tumefanya tathmini na kubaini hilo ndiyo tukafikia uamuzi huo," anasema.

Anasema, chama chake hakioni sababu za kupoteza muda na fedha kwa ajili ya kuweka mgombea, badala yake kitaunga mkono mgombea wa CCM ambaye kinaamini atakuwa ni Magufuli tu.

Mwenyekiti huyo anataja sababu nyingine kuwa Rais Magufuli amefanya mambo makubwa hivyo haiwezekani wakashindana naye na kuanza kupoteza rasilimali za umma bure.

"Ukimtoa Nyerere, JPM kaupeleka uchumi wetu mbele zaidi, vilevile viongozi wote wamefanya mambo, lakini huyu wa sasa ndiye aliyepaisha uchumi wa Tanzania, ni muhimu aungwe mkono," anasema.

Anasema, viongozi wote wamefanya mambo, lakini rais Magufuli ndiye aliyepaisha uchumi wa Tanzania, na kwamba huyo ni rais muhimu hata kwa TLP na Watanzania wengine wapenda maendeleo.



Mrema (kulia), chama chake kinatarajia kumtangaza Rais JPM kuwa mgombea anayeungwa mkono na chama hicho kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. **PICHA: MTANDAO.**

# TLP kumpitisha JPM kugombea urais 2020

- Yaeleza chama hakina mwenye kiwango chake

> Ukimtoa Nyerere, JPM kaupeleka uchumi wetu mbele zaidi, vilevile viongozi wote wamefanya mambo.

Anasema, TLP imeangalia upepo wa kisiasa na kuona kuna haja ya kumuunga mkono ili aendelee kuongoza na kwamba kama CCM isingempitisha kuwania urais, katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 isingeambulia kitu.

Anasema, inawezekana uamuzi huo wa kuunga mkono mgombea wa CCM ukawashangaza wengi, lakini anasisitiza kuwa ni kutokana na kukosa mgombea mwenye viwango na pia kuridhishwa na utendaji wa Magufuli.

"Aidha, nimpongeze kwa busara zake na hekima kutokana na jinsi alivyofanya uamuzi wa kihistoria wa kukutana na viongozi wa upinzani Ikulu na kuzungumza nao," anasema.

Mwenyekiti huyo anasema, baadhi ya wanasiasa walikuwa wakidai rais hapendi upinzani, na kwamba kitendo chake cha kukutana nao Ikulu kimeonyesha ni jinsi gani anapenda demokrasia.

**HAKUNA UBIA ZAIDI**

Mrema anasema, ubia wa chama chake na CCM ni kwenye nafasi ya urais tu na kwamba katika nafasi za ubunge na udiwani watachuana kama kawaida, hivyo CCM wasitarajie mteremko.

"TLP itajikita zaidi kwenye nafasi za ubunge na udiwani na kumwachia urais, huko ndiko kwenye ubia, lakini ubunge na udiwani tutapambana na hadi kieleweke, hivyo CCM wasitarajie mteremko," anasema.

Anasema, kwa sasa chama hicho kina madiwani wawili na hakina mbunge, hivyo, katika uchaguzi mkuu ujao kimejipanga kuhakikisha kinaweka wagombea wa kutosha kwenye nafasi hizo.

"Inawezekana wapinzani wenzetu wakatudharau, lakini wajue kuwa ubia wetu na CCM ni kwenye urais tu na tunatarajia kuonyesha upinzani kwenye ubunge na udiwani, hivyo hatuna mzaha katika hilo," anasema.

**KUUMUUNGA MKONO JPM**

Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, chama chake kilimweka mgombea wa urais wa TLP, Maximillian Lyimo, huku yeye (Mrema) akiwania ubunge wa jimbo la Vunjo mkoani Kilimanjaro, lakini wakati kampeni zikiendelea, katika hali isiyotarajiwa, Mrema aligeuka na kumpigia debe mgombea urais wa CCM na kumwacha wa chama chake.

Aidha, katika uchaguzi huo, Mrema hakushinda ubunge na badala yake jimbo likachukuliwa na mgombea wa Chama cha NCCR-Mageuzi ambaye ni mwenyekiti wa chama hicho taifa, James Mbatia.

Wakati huo yawezekana uamuzi wa kuunga mkono mgombea wa CCM uliokuwa wa Mrema peke yake, lakini sasa kimekuja nao kupitia vikao, lakini chama kikisisitiza kuwa ni lazima mapambano yawepo kwenye ubunge na udiwani.

## Uhuru wa habari uheshimiwe uchaguzi mkuu

Ukurasa 12

# Uhuru vyombo vya habari uheshimiwe uchaguzi mkuu



Zana mbalimbali za wanahabari. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Salome Kitomari**

OKTOBA mwaka huu, Tanzania itafanya uchaguzi wa madiwani, wabunge, wawakilishi, marais wa Zanzibar na wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Uchaguzi unafanyika baada ya miaka mitano kupita, ili kupata viongozi wapya wa kuongoza kwa miaka mitano mingine hadi 2025.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Nec), imepewa wajibu wa kusimamia uchaguzi uhuo ikiwamo kutoa ratiba yaani kupuliza kipenga, kwa kutangaza majina ya wagombea, kuwathibitisha na kusimamia mchakato wa uchaguzi.

Kwa sasa vyama viko katika hatua mbalimbali za maandalizi ingawa bado kipenga hakijapulizwa kwa ajili ya kuanza uchaguzi huo ambao kwa mujibu wa katiba hufanyika kila Jumamosi ya mwisho ya mwezi Oktoba.

Vyombo vya habari vina wajibu mkubwa wa kuhabarisha umma juu ya ahadi za wagombea na jinsi kampeni zinavyofanyika na mambo yote yanayohusiana na uchaguzi mkuu.

Wakati wa uchaguzi kila mmoja anataka kuhakikisha anashinda uchaguzi hasa kile anachogombea, hivyo kila mgombea hufanya analoweza kwa juhudi zote ili aweze kuibuka mshindi, na ndipo hutokea mchezo mchafu na siasa za majitaka.

> Hakuna asiyetambua kuwa uhuru unapaswa kuwa na mipaka, na siyo kwamba wanahabari au jamii inataka uhuru ambao unavuka mipaka na ndiyo maana kuna sheria zinazowaongoza.

Kipindi hicho vyombo vya habari vinapaswa kutimiza wajibu wake wa kuhabarisha umma kwa kila kinachoendelea kwenye kampeni hizo bila upendeleo wowote.

Aidha, ni wakati huo ndipo vyombo vya habari huingia kwenye mitego na lawama za wanasiasa ambao hupenda magazeti, runinga na redio kuwapamba na kuwapendezesha wao bila kujua wanafanyakazi hiyo kwa kuendeshwa na taaluma yao.

Kwa kawaida jicho la mwandishi wa habari siyo jicho la msomaji au mtu ambaye hana taaluma ya habari, na ndiyo maana ili uwe mwanahabari ni lazima ukasome na kujifunza taaluma hiyo na kuhitimu vyema.

Imekuwa bahati mbaya wanasiasa wengi hupenda kuwapangia wanahabari waandike nini kwa wakati gani kwa manufaa yao wenyewe, baadhi huwa hawajali wala kuheshimu taaluma hiyo ambayo wapo wanaoiita mhimili wa nne.

Ibara ya 18 ya Katiba imetoa uhuru wa kujieleza na kupokea taarifa ambayo ndiyo inayowapa nguvu waandishi wa habari kuandika kile ambacho ni habari kilichojegwa katika misingi ya ukweli na maadili ya taaluma yao.

Pia zipo sheria za Huduma za Habari ya mwaka 2016 na ya Haki ya Kupata Taarifa, ambazo zote ni kwa ajili ya wanahabari na jamii kwa ujumla, na kutokana na sheria hizo ndipo uhuru wa kujieleza unapaswa kuheshimiwa na wanasiasa.

Katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu ni lazima wanasiasa watambue kuwa taaluma ya habari haipaswi kuingiliwa kwa namna yoyote, na kama kuna kosa la kitaaluma lililofanywa na mwanahabari linapaswa kuangaliwa kama limekwenda kinyume na sheria zilizopo na kuchukua hatua kwa kwenda mahakamani.

Wanasiasa wasiwe wepesi wa kuumiza wanahabari na kuwakandamiza hasa wakati wa kampeni.

Haitarajiwi uhuru wa kujieleza kuendelea kuminywa wakati huu wa kampeni, vyombo vya habari na waandishi wa habari waachwe wawe huru kuripoti kile ambacho ni habari, kwa kuwa yote wanafanya kwa kuzingatia katiba, sheria na taratibu za nchi.

Hakuna asiyetambua kuwa uhuru unapaswa kuwa na mipaka, na siyo kwamba wanahabari au jamii inataka uhuru ambao unavuka mipaka na ndiyo maana kuna sheria zinazowaongoza.

Ubaya wa kuminya uhuru wa kujieleza na kuwaziba midomo na mikono wanahabari ni kuwa na jamii ambayo haina taarifa za kutosha, na wananchi hawatapata ukweli wa ahadi zinazotolewa na wagombea.

Kipindi hicho ndicho cha wananchi kudanganywa kwa ahadi nyingi ikiwamo za kuhamisha milima wakati ni kitu kisichowezekana na ndipo utaona wengi wakijitokeza na ahadi za kukifanya kijiji flani kufanana na New York iliyojengwa tangu karne ya 18, lakini ahadi huwa ni kuwa ndani ya miaka mitano kutakuwa na mabadiliko makubwa.

Wapo ambao hadi sasa hawajatimiza ahadi za mwaka 2015 na leo hii wakiulizwa wapiga kura hao huenda wakawa wakali na kuagiza wachukuliwe hatua, na wakati huu ndipo vyombo vya habari vitakumbusha ahadi hizo lakini vitaishia kupewa majina.

Hakuna ubishi kuwa, wakati huu wa kampeni waandishi hupewa vyama ambavyo wakati mwingine hawahusiki navyo na huenda hawajawahi kufikiri kuwa wanachama wa vyama husika, na wengine huumizwa kwa kupitia mitandao ya kijamii kwa kusingiziwa ambayo hawahusiki nayo.

Wanasiasa waepuke ubinafsi uliopindukia wa kupenda madaraka, wasikubali kuwatumia wananchi kuvuna fedha za nafasi hizo kwa kazi ambayo hawajafanya, kwa kuwa wapo wabunge ambao licha ya kuchaguliwa lakini hawajui kwanini wapo ndani ya muhimili huo na uwakilishi wao hautoshelezi.

Uhuru wa wanahabari na vyombo vya habari uheshimiwe wakati huu wa kampeni kuliko kuwatumia na kuwaumiza kwa sababu za manufaa ya kujijenga kisiasa.

# Mwaka mmoja mapinduzi Sudan, hali bado ni tete

Na Mwandishi Wetu

APRILI 9, mwaka huu umetimia mwaka mmoja baada ya kutimuliwa madarakani rais wa zamani wa Sudan Omar al Bashir.

Sudan imeuadhimisha mwaka mmoja wa mapinduzi dhidi ya Bashir tangu kuondolewa kwa dikteta huyo kimya kimya. Hakuna cha kusherehekea.

Uchumi bado uko dhaifu, hali ya kisiasa bado ni tete, wakati janga la COVID-19 linazusha mtafaruku mwingine kwenye taifa hilo ambalo halijasimama.

Mwaka mmoja uliopita, maelfu ya raia wa Sudan walifanya maandamano ya wiki nzima mbele ya makao makuu ya jeshi katika mji mkuu wa nchi hiyo Khartoum, kutaka ang'atuke.

Mwanafunzi kijana mwanamke , Alla Salah , alisimama juu ya paa la gari akiimba kauli mbiu za kisiasa, baadaye alikuja kuwa ishara ya vuguvugu la maandamano katika jamii ambayo kwa kiasi kikubwa inadhibitiwa na wanaume zaidi.

Kila mmoja aliingia mitaani, ikiwa ni pamoja na maprofesa, walimu na madaktari. Wasanii waliandika ujumbe na kuchora picha za uhuru katika kuta mjini Khartoum.

Kwa miezi kadhaa, nchi hiyo ilikuwa ikiwaka moto hadi hatimaye kile ambacho hakukufikirika kikatokea nacho ni dikteta Omar al-Bashir kupinduliwa Aprili 11, 2019, baada ya karibu miongo mitatu madarakani.

Yalikuwa mapinduzi yaliyoelezwa na wengi kuwa ni vuguvugu la mapinduzi ya mataifa ya Kiarabu namba mbili. Raia walijisikia furaha kubwa baada ya kufanikiwa kumng'oa.

Lakini mwaka mmoja baadaye, katika kusherehekea mwaka mmoja wa siku hii kubwa, hali mjini Khartoum imenyong'onyea na watu wako taabani.

Ni kwa sababu ya janga la virusi vya corona, shule na vyuo vikuu vimefungwa. Sherehe za maadhimisho , kupeperusha bendera na kuimba wimbo wa taifa ama nyimbo za mapinduzi, ni mambo yaliyofanyika nyumbani ama katika mitandao ya kijamii.

Lakini kuna sababu nyingine ya hali hiyo ya kunyong'onyea kwani baada ya miezi 12 ya uhuru wa kisiasa , Sudan haijapiga hatua ambayo ilipigiwa matumaini.

Nchi hiyo iko imara kisiasa lakini tete. Uchumi wake umeporomoka kabisa, na janga la virusi vya corona , linatishia kuharibu mafanikio madogo nchi hiyo iliyoyapata katika miezi 12 iliyopita kwenye harakati za kufufua biashara na uchumi.

Sudan ni mshirika muhimu katika eneo la kanda hiyo. Ni nchi ya tatu kwa mkubwa katika bara la Afrika, pamoja na watu wake milioni 42 inaonekana kuwa ni daraja kati ya Afrika na dunia ya Kiarabu. Sudan pia ni moja kati ya nchi muhimu za kupitia watu wanaokwenda kusaka uhamiaji kutoka bara la Afrika.



Alla Salah juu ya gari, akiimba kaulimbiu za kisiasa ya mabadiliko, ndiye mhamasishaji wa vuguvugu la maandamano nchini Sudan ambalo limetimiza mwaka mmoja. **PICHA: DW**

> Changamoto za kipindi hicho cha mpito cha miaka mitatu ni sawa na zile zilizochangia kuanguka kwa serikali ya al-Bashir, anaelezea Magdi al-Gizouli, mtafiti katika taasisi ya Rift Valley.

Iwapo hali ya kisiasa na kiuchumi itakuwa bora , Sudan inaweza kutoa fursa ya uwekezaji kutoka nje, kwa mfano katika sekta ya mafuta na kilimo.

Lakini kwa hivi sasa , Sudan imelala, na kutishia kuleta madhara makubwa kutokana na hali hiyo kwa eneo la kanda hiyo, anasema Philipp Jahn , Mkuu wa Kituo cha Utafiti wa Wakfu wa Friedrich Ebert nchini Sudan.

Licha ya mabadiliko chanya ya kisiasa , Sudan haikuweza kufanya yale yaliyokuwa yakitazamiwa

**HISTORIA**

Dikteta Omar al-Bashir, aliyechukuwa madaraka mwaka wa 1989 kupitia mapinduzi ya kijeshi, alihukumumiwa kwa mara ya kwanza Desemba 2019 na hivi sasa yuko gerezani mjini Khartoum.

Mmoja wa viongozi wa serikali ya mpito alielezea mapema Februari kwamba serikali inataka kumkabidhi Bashir katika Mahakama ya Kimataifa ya Jinai ya ICC huko Uholanzi, zaidi ya muongo mmoja tangu kuitolewa waranti ya kukamatwa kwake iliyotolewa na mahakama hiyo kwa tuhuma za uhalifu dhidi ya ubindamu uliofanywa katika jimbo la Darfur, lakini utaratibu huo haujawekwa wazi.

Baada ya tofauti nyingi mwaka 2019 baina ya jeshi na viongozi wa waandamanaji, baraza la kitaifa la mpito liliundwa baina ya raia na wanajeshi ili kufuatilia serikali ya mpito kwa ajili ya uchaguzi utakaorejesha madaraka ya kiraia.

Changamoto za kipindi hicho cha mpito cha miaka mitatu ni sawa na zile zilizochangia kuanguka kwa serikali ya al-Bashir, anaelezea Magdi al-Gizouli, mtafiti katika taasisi ya Rift Valley.

Miongoni mwa changamoto hizo ametaja, mageuzi ya kisiasa, mzozo wa kiuchumi na kuboreshwa kwa hali ya maisha ya wananchi. Mzozo sugu wa kiuchumi umedhihirika nchini Sudan, ambao umesababisha nchi hiyo kutopiga hatua kwenda mbele kufuatia miongo mitatu ya uongozi wa kimabavu.

Katika nchi hiyo ambayo kupanda kwa bei ya mkate kulisababisha maandamano yaliyoipinduwa serikali ya Bashir, matatizo ya kiuchumi yameuweka hatarini ustawi wa kisiasa. Agosti 2019, Sudan iliunda serikali ya wasomi kufuatia makubaliano ya ugavi wa madaraka baina ya jeshi na viongozi wakuu wa upinzani.

**CHANGAMOTO ZA SASA**

Mtaalamu wa zamani wa kiuchumi katika Umoja wa Mataifa (UN), Abdallah Hamdok, aliteuliwa kuwa Waziri Mkuu. Miongoni mwa changamoto anazokumbana nazo ni kuporomoka kwa thamani ya faranga ya Sudan kwa asilimia 70, deni kubwa la taifa hilo na mazungumzo ya amani na waasi wa Darfur, magharibi mwa nchi.

Mzozo huo uliozuka mwaka 2003 baina ya jeshi na makundi ya waasi ya kikabila ulisababisha watu 300,000 kuuliwa na wengine 2,000,500 kuyahama makazi yao, kwa mujibu wa taarifa za Umoja wa Mataifa.

Mwaka 2011, Sudan ambayo ilikuwa katika hali ngumu ya kiuchumi kutokana na vikwazo vya Marekani, ilijikuta pia imegawanyika kutokana na kujitenga kwa Sudan Kusini, yenye utajiri wa mafuta na iliyojitangazia uhuru wake.

Marekani iliondoa vikwazo vyake vya kiuchumi dhidi ya Sudan mwaka 2017 baada ya miaka 20, hali hiyo iliwapa matumaini viongozi wa nchi hiyo kwa ajili ya kuweko na uwekezaji kutoka nje.

Miezi ya hivi karibu serikali ya mpito ilikumbana pia na changamoto hasa za kiusalama kufuatia jaribio la mauaji ya Waziri Mkuu mwezi uliopita.

Huko Darfur bado makabiliano ya umwagaji damu yanaendelea baina ya makundi ya kikabila licha ya serikali kuanzisha mazungumzo na makundi ya waasi ya Kordofan kusini na Blue Nile.

# Aliyoasisi Sokoine miaka 36, fikra zimebaki palepale



Sokoine akimpokea Rais wa China, Li Xiannian , kwenye uwanja wa ndege wa Dar-es-Salaam, alipofanya ziara nchini mwaka 1979. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Gaudensia Mngumi**

TAREHE 12 Aprili, 1984 hadi leo imetimia miaka 36. Hiyo ndiyo siku iliyokuwa mwisho wa maisha ya Waziri Mkuu wa zamani, Edward Moringe Sokoine, ambaye ametimiza miongo mitatu tangu alipofariki dunia.

Alimaliza safari yake duniani katika ajali ya gari iliyotokea mkoani Morogoro akiwa njiani kurejea Dar es Salaam, baada ya kumaliza kikao cha bunge na kukagua miradi ya maendeleo.

Taarifa za kufariki kwa Waziri Mkuu kijana tena aliyekuwa tayari kutumikia taifa ziliwaduwaza wengi kwa sababu alikuwa mhimili mkuu katika mchakato wa kuandaa mabadiliko ya kiuchumi na kupambana na ulanguzi na uhujumu uchumi kwa ajili ya manufaa ya Watanzania wote.

Habari za kifo chake ambazo zilitikisa taifa ziliwastua Watanzania wa kada mbalimbali popote wakiwamo wanasiasa, wakulima, wahadhiri wa vyuo vikuu, wanahabari, walimu shuleni na wanafunzi, iwe sekondari na vyuo vikuu kutokana na mchango wake mkubwa katika kuandaa taifa lenye uadilifu na uzalendo.

Wengi hawatasahau Aprili 12, mwaka 1984 Rais Julius Nyerere kwa masikitiko makubwa, alipotangaza kifo cha Sokoine akisema: "Watanzania wenzangu, ndugu yetu, kijana wetu, Waziri Mkuu, Edward Moringe Sokoine, amefariki dunia kwa ajali ya gari iliyotokea huko Dakawa nje kidogo ya mji wa Morogoro akitokea Dodoma kulihutubia bunge. Ajali hiyo ilitokea wakati alipokuwa katika ziara yake ya kukagua mashamba ya mahindi katika mkoa wa Dodoma na Morogoro. Msafara wa Waziri Mkuu ulivamiwa na gari aina ya Toyota Land Cruiser iliyokuwa ikiendeshwa na mkimbizi mmoja wa kutoka Afrika ya Kusini kwa jina Dumisani Dube ambaye alikuwa anaishi kwenye kambi ya wakimbizi ya Mazimbu mjini Morogoro. Dube alisimamishwa na polisi lakini alikaidi na kwa vile alikuwa katika mwendo mkali akasababisha ajali kwa kuigonga gari aina ya Mercedes Benz iliyokuwa imembeba Waziri Mkuu na kusababisha kifo chake.

Watanzania wenzangu nawaombeni sana mkubali kwamba Waziri Mkuu Edward Moringe Sokoine amefariki kwa ajali ya gari", alimalizia.

> Wakati tunasherehekea na kufurahia maisha na uongozi bora uliotukuka wa Sokoine, tunamsifu na kumshukuru Mungu.

Watanzania walishikwa na butwaa na wengi hawakuamini taarifa hiyo kwa sababu katika kipindi hicho, mawazo ya wengi wote yalielekezwa katika kupambana na ulanguzi na kudhibiti wahujumu uchumi pamoja na kusisitiza kampeni ya nguvu kazi iliyokuwa inamhimiza kila mmoja kufanyakazi.

Hata hivyo, wengine walianza kuamini kuwa ni kweli Sokoine amefariki pale mwili wa mwanamapinduzi huyo ulipowasili kutoka Morogoro na kufikishwa katika hospitali ya jeshi iliyoko kambi ya jeshi ya Ngerengere kwa ajili ya maandalizi ya kupeleka Dar es Salaam.

Inakumbukwa kuwa Sokoine alivamiwa na kugongwa na gari lililodaiwa kuendeshwa na raia wa Afrika ya Kusini Dumisani Dube eneo la Dakawa na kusababisha kifo chake lakini zama hizo hakukuwa na msafara wala ulinzi kama ilivyo zama hizi.

Sokoine aliyezikwa nyumbani kwao Monduli mkoani Arusha, Watanzania wanakiri kuwa alikuwa mtu aliyefanya kazi zake bila hofu na muda wote alitimiza wajibu akitamani kuwa na mageuzi ya kiuchumi na uadilifu kwa maendeleo ya taifa.

Tanzania inapomkumbuka Sokoine, inashukuru viongozi na serikali kwa kupambana na ufisadi na tamaa za wachache kutaka kujinufaisha na mali za taifa kuanzia kusaini mikataba mibovu ya kuwatajirisha wachache wakiwamo wageni. Kinachoendelea ni kufanikisha mapambano na maono ya baba mpendwa Sokoine ambayo yalitamani Tanzania iwe kwa manufaa ya wote.

Mioyo ya Watanzania inaendelea kumlilia Sokoine lakini hakuna la kufanya japo watafarijika zaidi wakiona watoto wa taifa hili wanasoma sana kama Sokoine alivyotamani.

Wakishuhudia kila kunapotolewa huduma ya afya kuanzia zahanati, kituo cha afya hadi hospitali za rufani na taifa kuna dawa na wananchi wanatibiwa.

Mambo ni mengi katika kumuenzi Sokoine na mojawapo ni wananchi kushirikiana na vyombo vya usalama kufichua mitandao ya unyama na mauaji pia kuachana na mienendo inayoliumiza taifa na mojawapo ni kushirikiana na wahalifu wakiwamo wezi, wahujumu uchumi, mafisadi na wawekezaji wenye nia ya kuibia taifa rasilimali zake.

Katika kumkumbuka Sokoine, ni vyema kuwa na hofu ya Mungu, hivyo ni wakati wa kusimama kama taifa na kushikamana kuwa na uzalendo na kukataa uovu unasababisha watu wengi kuwa maskini.

Aidha, ni ukweli kuwa, Sokoine alikuwa mtu muhimu sana kwa nchi hii hasa kwa mchakato mzima wa kufanikisha mabadiliko ya kiuchumi na hasa kupambana na rushwa na ulanguzi.

Kifo cha Sokoine hakitasahaulika kutokana na ujasiri wake katika masuala ya siasa, uchumi na kutafuta haki kwa wale wanaopokwa haki zao, tena alikuwa mtu mwadilifu kiasi kwamba hata maisha yake yalikuwa ya kawaida mno pamoja na kuwa alikuwa kiongozi mkuu wa serikali.

Sokoine hakuwa mwoga kutoa mawazo yake kwa kile alichokiamini, wakati wa uhai wake alikuwa anachukia rushwa, dhuluma na mtu aliyechukia maovu, jambo ambalo liliwafanya viongozi wengine kumheshimu na kuamini mambo aliyokuwa akiyaamua hasa mazito ya kitaalamu na yale yanayohusiana na mustakabali wa siasa za taifa.

Sokoine anaheshimika kwani alikuwa mzalendo, jasiri na mwanamapinduzi wa kifikra katika utendaji, kusimamia kazi na kuongoza umma uliokuwa nyuma yake, mwili umeondoka juu ya nchi, lakini nafsi yake , kazi zake na jitihada zitabaki kama mhimili wa moja ya karama kubwa za uongozi wa taifa hili.

Alikuwa mtu asiyehesabu wala kujali mapato zaidi ya kutanguliza uzalendo, utu utaifa na utumishi uliotukuka. Wakati huzuni ikiwa bado ndani ya mioyo ya watoto wake, wake zake , jamaa zake, wajukuu na wote waliomtegemea na kumpenda, umma ungependa kuona ufisadi, rushwa, uhujumu uchumi, ulanguzi na unyonyaji aliouchukia Sokoine ukidhibitiwa.

Daima Sokoine atakumbukwa kwa kulitetea taifa na kuwapigania Watanzania.

Wakati tunasherehekea na kufurahia maisha na uongozi bora uliotukuka wa Sokoine, tunamsifu na kumshukuru Mungu.



## Rungwe watakiwa vita utapiamlo, udumavu

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

WANANCHI kwa kushirikiana na viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, wametakiwa kuwa mstari wa mbele kukabiliana na tatizo la utapiamlo pamoja na udumavu dhidi ya watoto ambalo linasababishwa na ukosefu wa lishe bora.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Wilaya hiyo, Julius Challya, wakati wa mahojiano na Nipashe juu ya mikakati iliyowekwa katika kukabiliana na tatizo la utapiamlo na udumavu licha ya kuzalisha chakula kwa wingi.

Alisema miongoni mwa mikakati iliyowekwa na wilaya hiyo ni kutoa elimu kwa wananchi namna ya kuandaa chakula lishe kwa watoto ambapo maofisa afya wa vijiji na kata walianza kufanya hivyo.

Alisema licha ya Serikali kuanza kutoa elimu kwa wazazi na walezi namna bora ya kuandaa chakula lishe kwa kuzingatia makundi ya vyakula, lakini wana jukumu la kuhakikisha wanazingatia ushauri wa kitaalamu katika kuwahudumia watoto wao.

"Miongoni mwa sababu zinazochangia tatizo la udumavu kwa watoto wetu ni wazazi kutokujua namna ya kupangilia na kuzingatia makundi ya vyakula, badala yake kutumia aina moja ya chakula kila siku, jambo ambalo linadidimiza afya na ukuaji wa watoto," alisema Challya.

Ofisa Afya wa Mkoa wa Mbeya, Mashaka Juma, alibainisha kuwa watoto wanaoongoza kuwa na udumavu na utapiamlo ni watoto wa watumishi na wafanyakazi ambao baadhi yao hukosa muda wa kuhudumia familia.

Alisema mara nyingi jukumu la kuwahudumia watoto linafanywa na wafanyakazi wa ndani, ambao hawawezi kuwahudumia watoto ipasavyo, ikiwamo kuwapa lishe bora.

"Kwa kawaida, watoto lazima wanyonye mara 12, hii inasaidia kupata virutubisho muhimu vya kujikinga na magonjwa na kuwa na afya njema, lakini baadhi ya watoto wa watumishi wanakosa vitu hivyo hali inayosababisha udumavu," alisema Juma.

Mmoja wa wakazi wa wilaya ya Rungwe, Butusyo Mwaijande, alisema moja ya mambo yanayosababisha tatizo la utapiamlo na udumavu ni wananchi kupenda kuuza mazao yao yote bila kubakisha akiba kwa ajili chakula kwa familia zao.

# Mazishi Kyela kufanyika asubuhi

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

MKUU wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, Claudia Kitta, amepiga marufuku mikusanyiko ya watu kwenye misiba na kuagiza mazishi yafanyike majira ya asubuhi ikiwa ni jitihada za kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona yanasababisha ugonjwa wa COVID-19.

Kitta alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha kujadiliana namna watakavyokabiliana na ugonjwa wa COVID-19 ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wananchi pamoja na kuweka ulinzi kwenye mpaka wa Kasumulu unaotenganisha Tanzania na Malawi.

Alisema suala la kuzuia mikusanyiko kwenye misiba na mazishi kufanyika majira ya asubuhi litasimamiwa na viongozi wa kata na vijiji na kuwahimiza kulisimamia jambo hilo kwa karibu zaidi ili kuepusha maambukizi.

"Ni wakati wa kupunguza au kuondoa mambo yanayoweza kuhatarisha usalama wetu... kuanzia sasa tuondoe mikusanyiko kwenye misiba na ingefaa zaidi mazishi yafanyike majira ya asubuhi, hii itasaidia kukabiliana na maambuzi ya virusi vya corona, nawaomba watendaji wote tulisimamie hili," alisema Kitta.

Aidha, Kitta aliwatoa hofu wananchi juu ya ugonjwa huo, na kuwakumbusha kuzingatia na kufuata ushauri wa kitaalamu sambamba na kueleza changamoto ya maji wilayani humo kuwa kikwazo kwa wakazi hao kutokunawa maji mara kwa mara. Aliongeza kuwa, Serikali imetoa vifaa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kisima kikubwa cha maji ambacho kitasaidia kupunguza tatizo la maji wilayani humo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Ipinda, Dk. Hunter Mwakifuna, alimuhakikishia Mkuu wa Wilaya kuwa madiwani wote wataendelea kutoa elimu kwa wananchi wao namna ya kujikinga na ugonjwa huo hatari wa COVID-19.



Baadhi ya watoto ambao ni wanafunzi wa shule mbalimbali za msingi na sekondari, wakisaidia kazi za nyumbani kwa kutafuta kuni, katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya juzi, kutokana na Serikali kuzifunga shule zote ili kuepuka maambukizi ya virusi vya corona. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Kizimbani kwa tuhuma za kubaka mtoto

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi, Mkoa wa Mbeya, imempandisha kizimbani mshtakiwa Francis Mlingano (24), kazi wa Kalobe kwa tuhuma za kumbaka binti mwenye umri wa miaka 13 pamoja na wizi wa mali mbalimbali, ikiwamo televisheni.

Akisoma maelezo ya awali yanayomkabili mshtakiwa huyo, mbele ya Hakimu Mkazi wa Mkoa huo, Andrew Scout, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Wakili Baraka Mgaya, alidai mtuhumiwa alitenda makosa Februari 14, mwaka huu.

Wakili Mgaya alidai siku hiyo mshtakiwa aliende nyumbani kwa wazazi wa binti aliyefanyiwa kitendo cha ukatili (jina linahifadhiwa) eneo la Nzovwe na kumkuta akiwa amelala ndipo alimbaka.

Aliendelea kuieleza mahakama kuwa, mtuhumiwa alifanya kitendo hicho wakati wazazi wa binti wakiwa kazini, kosa ambalo alidai ni kinyume cha kifungu namba 130 (1), (2) E na kifungu namba 131 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.

Wakili Mgaya aliongeza kuwa, baada ya kutimiza haja yake, mshtakiwa Mlingano, aliiba televisheni moja yenye thamani ya Sh. 150,000 na deki moja yenye thamani ya Sh. 50,000.

Mshtakiwa alikana kutenda mashtaka yote mawili, lakini Wakili wa Serikali Mgaya, aliiarifu mahakama kuwa muathirika alieleza kumfahamu mhusika kwa sura baada ya kupata vipimo hospitali.

Hata hivyo Hakimu Scout aliahirisha kesi hiyo kwa ajili ya kuanza usikilizwaji upande wa Jamhuri kuwasilisha mashahidi ili kuithibitishia mahakama kuhusu tuhuma zinazomkabili Mlingano.

Mlingano alirudishwa mahabusu baada ya kukosa watu wa kumuwekea dhamana hadi hapo kesi itakapoendelea.



# Sera ya Elimu kuzingatia wanafunzi wenye ulemavu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema ipo katika hatua za mwisho kukamilisha Sera ya Elimu Mjumuisho ambayo itazingatia mahitaji yote ya wanafunzi wenye ulemavu.

Hayo yalisemwa na Kaimu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Mahmoud Thabit Kombo, wakati akitoa ufafanuzi na kujibu hoja za wajumbe wa kamati ya ustawi wa jamii.

Alisema Wizara ya Elimu ya Mafunzo ya Amali imeanzisha elimu ya mjumuisho kwa lengo la kuwawezesha wanafunzi wenye mahitaji maalumu ikiwamo wenye ulemavu kufaidika na sekta ya elimu kwa wote.

Alisema ni takriban miaka sita tangu wizara hiyo kuanzisha elimu ya mjumuisho huku mafanikio makubwa yakipatikana kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu kupiga hatua kubwa sekta ya elimu.

Kombo alisema kinachofanywa na wizara ni kutekeleza azma ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 yaliyotangaza elimu bure kwa wananchi wote huku makundi yote yakifaidika na sekta hiyo.

"Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ipo katika mchakato wa kukamilisha sera ya elimu mjumuisho ambayo itaweka mazingira mazuri kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu nchini kote," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi, Mwanaasha Khamis Juma, aliitaka wizara hiyo kuimarisha kitengo cha elimu mjumuisho kwa kuwapatia walimu elimu zaidi ambayo itawawezesha kusomesha wanafunzi wenye mahitaji tofauti.

Alisema wamefanya uchunguzi na kubaini mahitaji ya walimu wenye uwezo wa kusomesha wanafunzi wenye mahitaji maalumu hawatoshi, na matokeo yake baadhi ya shule wanafunzi wa aina hiyo hawafaidiki na fursa za elimu inayotolewa.

Alisema baadhi ya shule za vijijini hazina walimu wenye uwezo wa kusomesha wanafunzi wenye ulemavu wa kutoona na hivyo kuwafanya wazazi kuwabakisha watoto hao nyumbani.

"Wakati Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ikiimarisha elimu ya mjumuisho tunataka kuona kwamba walimu nao wanapatiwa mafunzo ambayo yatawawezesha kusomesha wanafunzi wa aina hiyo," alisema.



Naibu Waziri wa Afya Zanzibar, Harusi Said Suleman (kushoto), akipokea msaada wa vifaa vya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona, kutoka kwa Khadija Sharif wa Taasisi ya Milele Zanzibar, katika hafla iliyofanyika katika Wizara ya Afya, Mnazi Mmoja, juzi.
**PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# 'Msiwanyanyapae waliopona ugonjwa corona'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Hamad Rashid Mohamed, amewataka wananchi kuacha kuwanyanyapaa wagonjwa wa corona ikiwamo wale wanaopona na kurudi katika familia.

Alitoa ufafanuzi huo mbele ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na kusema ugonjwa huo umethibitisha kwamba unaweza kuwapata watu wa rika tofauti ikiwamo matajiri, masikini na watoto.

Alisema huu ni wakati wa kujenga mshikamano na upendo katika janga la ugonjwa wa corona na sio tabia ya kubaguana kwa kutengana.

"Wizara ya Afya inatoa tahadhari na kuwataka wananchi wasiwabague watu wanaougua ugonjwa wa corona na wale waliopona kwa sababu ugonjwa huo hauchagui...tumeshuhudia ugonjwa huu ukiwasubumbua watu wa rika tofauti," alisema.

Aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari ya ugonjwa huo ambao katika siku za hivi karibuni kumekuwa na maambukizi ya ndani ya nchi.

Alizitaja tahadhari hizo ikiwamo kuepukana na mikusanyiko katika maeneo mbalimbali ikiwamo sokoni na hotelini.

"Hivi sasa tumeanza kupata wagonjwa wa corona ambao ni wa humu ndani ikionyesha kwamba sasa maambukizi ya ugonjwa wa corona yameingia katika jamii jambo ambalo ni hatari kubwa," alisema.

Mapema Naibu Waziri wa Afya, Harusi Suleiman, aliwapongeza wafanyabiashara na taasisi mbalimbali ikiwamo sekta binafsi kwa kusaidia kutoa vifaa vya kupambana na ugonjwa huo.

Alisema hiki ni kipindi kizuri cha kujenga ushirikiano na kusaidia mapambano ya ugonjwa wa corona na kuona ugonjwa huo unatokomezwa nchini.

"Wizara ya Afya ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, inatoa shukrani za dhati kwa wafanyabiashara pamoja na taasisi za sekta binafsi kwa kusaidia mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona ambalo ni janga la kitaifa," alisema.

# Wakulima watakiwa kuitumia vizuri mvua ya masika

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAKULIMA wametakiwa kuitumia vizuri mvua ya masika inayoendelea kunyesha kwa kuotesha miche ya aina tofauti ya mazao ya kilimo licha ya kuwapo kwa janga la ugonjwa wa corona.

Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Dk. Makame Ali Ussi, alisema hayo wakati akifafanua mbele ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuhusu mvua ya masika inayoendelea kunyesha na wizara imejipanga vipi kutoa elimu kwa wakulima katika kipindi hiki ambacho taifa linakabiliwa na ugonjwa huo.

Alisema njia pekee ya kukabiliana na ugonjwa huo ni kwa wakulima kuongeza bidii ya kuzalisha vyakula mbalimbali ili kukabiliana na tatizo la njaa.

Alisema hiki ni kipindi kizuri kwa wakulima kuongeza bidii na kuzalisha vyakula vingi ikiwa ni hatua ya kuchukua tahadhari na janga la njaa wakati taifa likikabiliwa na ugonjwa huo.

"Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi inawataka wakulima kuendelea kuzitumia vizuri mvua za masika kwa kuotesha miche ya aina mbalimbali na vyakula vya mazao ili kuliwezesha taifa kupata chakula kingi zaidi," alisema.

Alizitaja juhudi zinazochukuliwa na Wizara ya Kilimo ni kusambaza kwa matrekta kwa ajili ya kusafisha mashamba ya mpunga kwa wakulima katika mabonde ya Unguja na Pemba.

Alisema hivi karibuni serikali imenunua matrekta 10 yenye uwezo wa kulima katika mazingira tofauti na hivyo kutoa fursa kubwa kwa wakulima kuendeleza kilimo cha mpunga.

"Matreka hayo tayari yapo mashambani kwa ajili ya kufanya kazi za wakulima, kusafisha mashamba yao ikiwa ni sehemu za maandalizi ya kilimo cha mpunga," alisema.

TANGAZO

# Spurs: Kane hauzwi EPL

**LONDON,** England

KLABU ya Tottenham Hotspur haina mpango wa kumuachia mshambuiaji wake, Harry Kane aondoke kipindi cha majira ya joto na hawatamuuza kwa wapizani wao wa Ligi Kuu ya England.

Kane mwenye umri wa miaka 26, alisaini mkataba wa miaka sita pale Spurs Juni mwaka 2018.



Mwezi uliopita alisema kwamba, hatasalia kwenye klabu hiyo ya London Kaskazini kwa sababu hiyo, na kuwa ripoti ikimnukuu Mwenyekiti, Daniel Levy, akisema kwamba amefungua milango ya kumuuza mchezaji huyo kwa euro milioni 200.

Levy alibainisha kwamba, wanaweza kumuuza mchezaji huyo, lakini si kwa wapizani wao wa Ligi Kuu ya England.

"Kama klabu yoyote ikifikia bei yetu ya euro milioni 200 tutamuuza bila shaka yoyote," alisema akinukuliwa na gazeti la Daily Mail.

Hata hivyo, mwenyekiti huyo alibainisha kwamba, hawatamuuza kwa timu wapinzani wao wa Ligi Kuu ya England.



# MBAPPE KUMRITHI MANE LIVER

**LIVERPOOL,** England

KLABU ya Liverpool, imeripotiwa kwamba inamfuatilia kwa karibu Kylian Mbappe kama watampoteza Sadio Mane kwenda Real Madrid.

Mane amejiimarisha kama mmoja wa washambuliaji bora duniani pale Liverpool, na sasa yupo kwenye orodha ya wachezaji wanaowaniwa na Real Madrid.

Lakini vinara hao wa Ligi Kuu ya England wanataka kulipwa fedha nyingi zaidi kama mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal ataamua kwenda pale Santiago Bernabeu. Madrid inafikiria kumsajili Mane na Liverpool sasa imewekeza nguvu kumtaka nyota wa Paris Saint-Germain, Mbappe kama mrithi wake, kwa mujibu wa gazeti la The Sun.

Ripoti hiyo imesema kwamba, Mane mwenyewe haonyeshi nia kubwa ya kutaka kuondoka pale Anfield.Mbappe mwenye umri wa miaka 21, amekuwa akihusishwa na 'Los Blancos', lakini pengine Liverpool wanaweza kumtwaa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa.

EQUITY

Equity Bank(Tanzania) Ltd

UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

WARAKA MIZANIA KWA TAREHE : 31 DESEMBA 2019

[illegible]

TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA 2019

[illegible]

TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2019

[illegible]

TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2019

[illegible]

## TANGAZO

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

**AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**
*benki kwa maendeleo yako*

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2019
## (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa sasa 2019 | Mwaka uliopita 2018 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 10,317 | 11,037 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 15,679 | 17,256 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 25,039 | 26,570 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 211 | 228 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 22 | 128 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | -4 | 0 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 0 | 0 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 84,745 | 82,996 |
| 12 | Mali Nyingine | 10,997 | 13,397 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 20 | 20 |
| 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 22,376 | 3,701 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **169,401** | **155,333** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 3,361 | 2,485 |
| 18 | Amana za Wateja | 107,111 | 116,273 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana Maalumu | 0 | 0 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 2 | 15 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 2,820 | 2,704 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 8 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 7,307 | 0 |
| 27 | Dhima Nyingine | 15,322 | 1,446 |
| 28 | Madeni | 12,086 | 10,500 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **148,010** | **133,431** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **21,391** | **21,902** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 10,984 | 8,607 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 4,688 | 7,547 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 0 | 0 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 5,719 | 5,748 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **21,391** | **21,902** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 372 | 978 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 16,706 | 21,604 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 9,204 | 17,280 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 1,461 | 1,491 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 12.6% | 14.1% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 17.8% | 21.4% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 83.9% | 83.6% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 55.5% | 64.6% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 64.9% | 70.5% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -7.0% | -21.2% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 9.1% | -14.9% |

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI
## KWA MWAKA ULIOISHIA 31.12.2019
## (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Limbikizo la Mwaka wa sasa 2019 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 2018 |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 29,265 | 28,721 |
| 2 | Gharama za Riba | -6,803 | -5,385 |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **22,461** | **23,336** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 0 | 0 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | -1,824 | -3,056 |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **6,211** | **7,987** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 349 | 90 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 5,039 | 7,077 |
| | 6.3 Gawio | 0 | 0 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 823 | 819 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **-28,074** | **-31,994** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | -14,645 | -16,000 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 0 | 0 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | -13,428 | -15,994 |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **-1,226** | **-3,727** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | -1,663 | 1,187 |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **-2,889** | **-2,540** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | 0 | 0 |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **-2,889** | **-2,540** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 429 | 456 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | -263 | -295 |
| 15 | **Idadi ya Matawi** | **18** | **18** |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -2% | -2% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -13% | -11% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 98% | 87% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 20% | 21% |

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31.12.2019

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2019** | **8,607,135** | **2,431,917** | **7,546,745** | **2,537,257** | **779,217** | **0** | **21,902,271** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | -2,888,636 | 0 | 0 | 0 | **-2,888,636** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Miamala na wanahisa | 2,377,281 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **2,377,281** |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | -749,687 | 749,687 | 0 | 0 | **0** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 779,217 | 0 | -779,217 | 0 | **0** |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2019** | **10,984,416** | **2,431,917** | **4,687,639** | **3,286,944** | **-** | **-** | **21,390,916** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2018** | **8,607,135** | **2,431,917** | **11,865,765** | **694,193** | **843,314** | **0** | **24,442,324** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | -2,540,053 | 0 | 0 | 0 | -2,540,053 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | -1,843,064 | 1,843,064 | 0 | 0 | 0 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 64,097 | 0 | -64,097 | 0 | 0 |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2018** | **8,607,135** | **2,431,917** | **7,546,745** | **2,537,257** | **779,217** | **0** | **21,902,271** |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA
## KWA MWAKA ULIOISHIA 31.12.2019
## (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Limbikizo la Mwaka wa sasa 2019 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 2018 |
|---|---|---|---|
| **I:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | -1,226 | -3,727 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | |
| | - Hasara Katika Mali | 5,604 | 1,567 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | -3,922 | 17,189 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | -3 | 103 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | -7,921 | -33,525 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 1,531 | 10,521 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | -599 | -632 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 3,865 | 748 |
| | - Kodi Iliyolipwa | 0 | 0 |
| | - Mengineyo (bainisha) | 2,208 | 2,367 |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | **(463)** | **(5,390)** |
| **II:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| | Gawio Lililopokewa | 0 | 0 |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | -427 | -374 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 3 | 0 |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | -7,393 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 |
| | Mengineyo (bainisha) | 0 | -584 |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | **(424)** | **(8,351)** |
| **III:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 2,377 | 0 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 0 | 0 |
| | Mengineyo (bainisha) | -2,450 | 0 |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **(73)** | **-** |
| **IV:** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | -960 | -13,740 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 19,584 | 33,325 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **18,624** | **19,584** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA MWAKA ULIOISHIA 31.12.2019

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| Jina | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| | | **27-Mar-20** |
| **1. Ernest Massawe** | | |
| **2. Dr. Josephat Lotto** | | **27-Mar-20** |




## HABARI MICHEZO

# BALOTELLI ATAKA KUTUA NAPOLI




**NAPLES,** Italia

MSHAMBULIAJI wa Brescia, Mario Balotelli amebainisha kwamba, angependa kuichezea timu ya Napoli kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Balotelli alijiunga na timu ya nyumbani kwake, Brescia Agosti mwaka jana, lakini alihusishwa na kutua pale Napoli.

Mchezaji huyo wa zamani wa AC Milan, Inter na Liverpool amesema alijaribu kujiunga na Napoli na akabainisha bado angependa kuhamia pale kwenye Uwanja wa San Paolo.

"Nilijaribu kujiunga na Napoli," alisema Balotelli akimuambia Fabio Cannavaro wakati wa mahojiano live kwenye mtandao wa Instagram juzi Jumatatu.

"Nitakuwa na wakati mzuri nikiwa pale mji wa Naples. Binti yangu atafurahia sana, kwa sababu ni shabiki wa Napoli.

"Namuimbia, 'Brescia, Brescia', lakini yeye anaipenda zaidi Napoli. Alifurahi sana nilipompeleka kwenye Uwanja wa San Paolo.

"Mara zote kuna hisia nzuri kuingia kwenye Uwanja wa San Paolo, ingawa kwa maoni yangu uwanja mzuri zaidi ni San Siro."

Balotelli amefunga mabao matano katika mechi 19 za Serie A msimu huu kabla ya ligi kusimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Balotelli mwenye umri wa miaka 29, ameichezea timu ya Taifa ya Italia mechi 36 na kwa mara ya mwisho alicheza mwaka 2018 na amesema anataka kurudi tena na ana mheshimu kocha, Roberto Mancini.



# Immobile awania rekodi ya Higuain

**ROME,** Italia

NYOTA wa Lazio, Ciro Immobile anaifikiria rekodi ya Gonzalo Higuain ya ufungaji mabao kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, wakati ligi hiyo itakapoanza tena.

Immobile tayari ameshafunga mabao 27 Serie A msimu huu wakati ligi hiyo iliposimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19).

Huku zikiwa zimebaki mechi 12 kumalizika kwa ligi hiyo, Immobile anakaribia rekodi ya Higuain ya kufunga mabao 36 kwa msimu mmoja kwenye Ligi Kuu ya Italia, ambayo aliiweka akiwa pale Napoli msimu wa 2015-16.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, ana matumaini ya kufikia rekodi hiyo, na ameiambia Sky Sport kwamba: "Sijui. Itategemea".

"Najifua kwa bidiiili kufanikisha lengo hili. Kila mmoja ana malengo yake. Litakuwa jambo zuri.

"Tutaona kitakachotokea wakati nitakaporudi tena uwanjani. Nitafanya kila niwezalo."

Immobile ameisaidia Lazio kukaa nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo, ikipitwa pointi moja na Juventus, wakati msimu uliposimamishwa.

# Wachezaji Bayern kukatwa asilimia 20 ya mishahara

**MUNICH,** Ujerumani

WACHEZAJI wa Bayern Munich wamekubali kukatwa asilimia 20 kwenye mishahara yao kutokana na ligi kusimamishwa.

Sky Sport imeripoti kwamba, kikosi chote kitakubali kupunguzwa kwa mishahara yao kwa ajili ya kuwasaidia wafanyakazi wengine wa klabu wakati huu wa mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19).

Baadhi ya wachezaji wenye majina makubwa wa Bayern, tayari walishatangaza kutoa michango yao binafsi kwa ajili ya janga hilo, huku Robert Lewandowski (pichani)akichangia euro milioni moja kupambana na gonjwa hilo.

Joshua Kimmich na Leon Goretzka, wao kila mmoja alichangia euro 500,000.

Fedha ambazo tayari zimepatikana ni euro milioni 2.5 na zitagawiwa kwa taasisi mbalimbali.

"Kila mmoja anaweza kusaidia, wote kwa kikubwa au kidogo," alisema Kimmich.



# MWALIMU COMMERCIAL BANK PLC

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

**Kutoka taarifa ya fedha iliyokaguliwa na kuidhinishwa na wakaguzi wa mahesabu**

| WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DISEMBA 2019 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Mwaka wa sasa 31-Disemba-2019 | Mwaka uliopita 31-Disemba-2018 |
|---|---|---|
| **A. MALI:** | | |
| 1. Fedha Taslimu | 264 | 213 |
| 2. Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 4,618 | 1,691 |
| 3. Uwekezaji katika Amana za Serikali | - | 1,125 |
| 4. Salio katika Benki nyingine na Taasisi za fedha | 40 | 52 |
| 5. Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6. Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7. Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8. Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9. Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 1,043 | 2,294 |
| 10. Uwekezaji katika Amana Nyingine | - | - |
| 11. Mikopo Halisi Iliyopo | 16,109 | 17,886 |
| 12. Mali Nyingine | 6,560 | 5,560 |
| 13. Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14. Akaunti za udhamini | - | - |
| 15. Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,214 | 1,874 |
| **16. JUMLA YA MALI** | **29,848** | **30,695** |
| **B. DHIMA:** | | |
| 17. Amana za Benki nyingine na Taasisi za fedha | - | - |
| 18. Amana za Wateja | 11,073 | 7,949 |
| 19. Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20. Amana Maalumu | - | - |
| 21. Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22. Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23. Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 602 | 729 |
| 24. Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25. Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26. Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27. Dhima Nyingine | 1,706 | 723 |
| 28. Madeni | - | - |
| **29. JUMLA YA DHIMA** | **13,381** | **9,401** |
| **30. MALI/(DHIMA) HALISI** | **16,467** | **21,294** |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA:** | | |
| 31. Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 30,912 | 30,912 |
| 32. Akiba ya Mtaji | - | 179 |
| 33. Mapato Yaliyobakizwa | (9,618) | (4,473) |
| 34. Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (4,827) | (5,503) |
| 35 Akaunti Nyingine za Mtaji | - | 179 |
| 36. Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37. JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **16,467** | **21,294** |
| **38. DHIMA ZISIZO DHAHIRI** | | |
| 39. Mikopo Chechefu | 279 | 124 |
| 40. Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 292 | 374 |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | - | 2,300 |
| **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| - Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 55% | 69% |
| - Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 1.8% | 2.0% |
| - Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 145% | 225% |
| - Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 55% | 59% |
| - Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 58% | 70% |
| - Ongezeko la Amana | -5% | 45% |
| - Ongezeko la Mali | -2% | -19% |

| TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DISEMBA 2019 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Disemba-2019 | Limbikizo la Mwaka Uliopita 31-Disemba-2018 |
|---|---|---|
| **I. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| Mapato (Hasara) Halisi | (4,812) | (5,489) |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - |
| - Hasara katika Mali | 1,710 | 2,192 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 3,104 | 5,831 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | - | (288) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 3,284 | (1,982) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (27) | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (764) | 721 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (973) | 121 |
| - Kodi Iliyolipwa | - | - |
| - Mengineyo | (270) | - |
| **Fedha Halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **1,252** | **1,106** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - |
| - Gawio Lililopokewa | - | - |
| - Ununuzi wa Mali za Kudumu | (55) | (520) |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| - Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | 625 |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 1,121 | - |
| - Mengineyo | - | (270) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **1,066** | **(165)** |
| **III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | - | - |
| - Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| - Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| - Mengineyo | 375 | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha** | **375** | **-** |
| **IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - |
| - Ongezeko / Punguzo Halisi katika Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu | 2,693 | 941 |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 1,585 | 644 |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 4,278 | 1,585 |

| TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DISEMBA 2019 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Mtaji wa Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Ziada nyingine | Tengo la Ziada ya Jumla | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 30,912 | (9,976) | - | 179 | 179 | 21,294 |
| Faida (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (4,827) | - | - | - | (4,827) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | 179 | - | (179) | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | 179 | - | - | (179) | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **30,912** | **(14,445)** | **-** | **-** | **-** | **16,467** |
| **Mwaka Uliopita** | - | - | - | - | - | - |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 30,912 | (4,120) | 114 | 204 | - | 27,110 |
| Faida (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (288) | - | - | - | (288) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | (5,503) | - | - | - | (5,503) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | (25) | - | (25) |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - |
| | - | 114 | (114) | - | - | - |
| | - | (179) | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **30,912** | **(9,976)** | **-** | **179** | **-** | **21,294** |

| TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DISEMBA 2019 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Disemba-2019 | Limbikizo la Mwaka uliopita 31-Disemba-2018 |
|---|---|---|
| 1. Mapato ya Riba | 2,936 | 3,253 |
| 2. Gharama za Riba | 547 | 572 |
| **3. Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **2,389** | **2,681** |
| 4. Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - |
| 5. Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (80) | 87 |
| 6. Mapata Yasiyo ya Riba: | 454 | 218 |
| 6.1 Faida (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za kigeni | 27 | 4 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 403 | 213 |
| 6.3 Gawio | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 24 | 1 |
| 7. Gharama Zisizo za Riba | 7,735 | 8,302 |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 3,337 | 3,523 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | - | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | 4,398 | 4,779 |
| **8. Faida (Hasara) ya Uendeshaji** | **(4,812)** | **(5,490)** |
| 9. Tengo la Kodi ya Mapato | 15 | 14 |
| **10. Faida (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | **(4,827)** | **(5,476)** |
| 11. Mapato Mengine Yaliyojumuishwa | - | (25) |
| **12. Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(4,827)** | **(5,501)** |
| 13. Idadi ya Waajiriwa | 59 | 62 |
| 14. Mapato kwa Hisa | -78 | -89 |
| 15. Idadi ya Matawi | 2 | 2 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | 0 | 0 |
| - Uwiano wa Faida kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | *-16%* | *-18%* |
| - Uwiano wa Faida baada ya kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | *-29%* | *-26%* |
| - Uwiano wa Matumizi Yasiyo na Riba na Mapato Ghafi | *289%* | *295%* |
| - Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | *12%* | *13%* |

**BAADHI YA MAELEZO**
**KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DISEMBA 2019**

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

| *Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| Richard L. Makungwa (Ofisa Mtendaji Mkuu) | ……………………. (Imesainiwa) | 14 APRILI 2020 |
| Selemani Kijori (Mkuu wa Fedha) | ……………………. (Imesainiwa) | 14 APRILI 2020 |
| Patrick Mashallah (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) | ……………………. (Imesainiwa) | 14 APRILI 2020 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya sheria ya benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| *Jina* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| 1/ Herman Kessy | ……………………. (Imesainiwa) | 14 APRILI 2020 |
| 2/ Ambrose Nshala | ……………………. (Imesainiwa) | 14 APRILI 2020 |

**Head Office**

**Mlimani Tower - Mezzanine Floor,**
**Sam Nujoma Road**
**P.O.Box 61002,**
**Dar es salaam**
**Phone: 022-2772954/7**
**email: info@mcb.co.tz**
**Customer Care No.:**
**0629331151|0629331755|0800750033**

**Mlimani Branch**
**Mlimani Tower - Ground Floor**
**Sam Nujoma Road**
**Dar es salaam**

**Samora Branch**
**Samora Avenue**
**Consolidated Holding Building Ground Floor**

**Regional Office - Morogoro**
**19, Plot E, Nkomo Street**
**Phone: +255 622 005 574**
**Morogoro**

**Regional Office - Mbeya**
**90, Plot L, Sokomatola Street**
**Phone: +255 766 903 575**
**Mbeya**

**Regional Office - Mwanza**
**18, Plot A, Kirumba Street**
**Phone: +55 788 138 238**
**Mwanza**



## HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# SOLSKJAER, PEP VITANI KWA UPAMECANO

**Arsenal nayo yajipanga wakati huu akiruhusiswa kuvunja mkataba RB Leipzig kwa pauni...**

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United na Manchester City zote zimevutiwa na huduma ya beki wa kati wa RB Leipzig, Dayot Upamecano, hivyo kuingia katika vita vya kuisaka saini ya Mfaransa huyo.

**Nyota huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 21, ameibuka kuwa mmoja wa mabeki bora wajao Ulaya, na anaelezwa kuwa katika orodha ya wachezaji wanaowindwa na makocha hao wawili, Ole Gunnar Solskjaer na Pep Guardiola.**

City, ukweli inatarajia kusajili mabeki wawili wapya wa kati wakati dirisha la usajili litakapofunguliwa tena, imeruhusu mabao 31 hadi sasa msimu huu ikiwa ni zaidi ya iliyoruhusu kwenye misimu miwili iliyopita(23, 27), na 10 zaidi kuliko vinara wa ligi hiyo, Liverpool.

City ilitumia soko la Januari, lakini haikufanikiwa kukamilisha mpango huo, ilitazama wachezaji kama beki wa Bournemouth, Nathan Ake, wa Inter Milan, Milan Skriniar, wa Shakhtar Donetsk, Mykola Matvyenko, pamoja na wawili wa Leicester, Jonny Evans na Caglar Soyuncu.

Mahasimu wao United, kadhalika, wanataka kuongeza beki mwingine wa kati, wakati huu Chris Smalling na Phil Jones mustakabali wao wa baadaye ukiwa hauna uhakika, na wamerudia kuhusishwa na beki wa kati wa Napoli, Kalidou Koulibaly.

Arsenal pia imekuwa ikihusishwa na Upamecano katika kipindi kilichopita, lakini inaye William Saliba atakayejiunga nao majira ya joto akitokea St Etienne pamoja na kuwa na nafasi ya kumsajili jumla Pablo Mari anayeichezea kwa mkopo akitokea Flamengo.

Kwa mujibu wa Sky Germany, kinda huyo anayevutia, Upamacano pia anajadiliwa sana na klabu kubwa Ulaya, ikiwamo Bayern Munich na zingine kubwa za Hispania.

Mazungumzo yapo katika hatua ya mwanzo kabisa na kuvutiwa bado hakujaiva, hata hivyo, na zaidi kutokana na kutoeleweka kwa hali ya kifedha kunakochangiwa na janga la virusi vya corona linaloitesa dunia kwa sasa.

RB Leipzig si miongoni mwa klabu za Bundesliga zinazohaha fedha kwa sasa, lakini nini kinachovutia kuhusu hali ya Upamacano, ni kwamba anaelekea kuingia mwaka wake wa mwisho katika mkataba wake na klabu hiyo na ana kipengele kinachomruhusu kuuvunja kwa pauni milioni 52.5.

Jambo ambalo litaifanya thamani yake kuwa sawa na ile ya Ake na mabeki wengine wanaotajwa kuwa na thamani kubwa England kama James Tarkowski wa Burnley na Lewis Dunk pale Brighton, na wakati dirisha la usajili likitarajiwa kufunguliwa Juni 10, mwaka huu licha ya kwamba hakuna tarehe rasmi iliyopangwa kwa kuendelea tena kwa msimu wa 2019/20.

Upamecano amecheza mechi 29 katika mashindano yote msimu huu, ikiwamo mechi sita za Ligi ya Mabingwa Ulaya, wakati huu RB Leipzig ikitoa msukumo kwa Bayern na Borussia Dortmund kileleni mwa Bundesliga. Kwa sasa ikiwa nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo, pointi tano nyuma wakati huu zikiwa zimebaki mechi tisa kabla ya msimu kumalizika.

## ZISIKUPITE

### REAL KWA HAALAND, MBAPPE

REAL Madrid ina mpango wa kumsajili mshambuliaji wa Norway, Erling Braut Haaland, 19, kutoka Borussia Dortmund mwaka huu pamoja na straika Mfaransa Kylian Mbappe, 21, kutoka Paris St-Germain hapo mwakani. ***(Marca)***

### DORTMUND KWA TORRES

BORUSSIA Dortmund imetoa ofa ya pauni milioni 34.9 kwa winga wa Hispania na Valencia, Ferran Torres, 20, ambaye ana kipengele kinachomruhusu kuvunja mkataba wake kwa pauni milioni 87 na mkataba unaomalizika mwaka 2021. ***(Bild, via Sport)***

### IGHALO KULIPWA £200,000

MSHAMBULIAJI wa Nigeria, Odion Ighalo, 30, atapaswa kupunguziwa mshahara wake na kulipwa pauni 200,000 kwa wiki kutoka pauni 300,000 alizokuwa akilipwa na Shanghai Shenhua kwa wiki kama anataka kusajiliwa jumla na Manchester United anayoichezea kwa mkopo akitokea klabu hiyo ya China. ***(Star)***

### LAMPARD AMTAKA BIRD

CHELSEA itapaswa kulipa pauni milioni tano kama itataka kumsajili kiungo wa Derby County, Muingereza Max Bird, 19, ambaye amemvutia kocha wa 'Blues' hao, Frank Lampard wakati akiinoa klabu hiyo ya Ligi Daraja la Kwanza ('Championship'). ***(Football Insider)***

### ONANA AZIVUTIA PSG, BARCA

PARIS St-Germain imejiunga na Barcelona katika kuonyesha nia ya kumsajili kipa wa Cameroon na Ajax, Andre Onana, 24. ***(L'Equipe - in French)***

### MBAPPE KUMRITHI MANE

ZINEDINE Zidane anataka kumsajili Sadio Mane majira ya joto na Liverpool inatazama uwezekano wa kuipata huduma ya Kylian Mbappe kama mbadala. ***(The Sun)***

### ARSENAL KUMKOSA JOVIC

REAL Madrid inapanga kumbakisha straika Mseribia, Luka Jovic, 22, ambaye anaivutia Arsenal. ***(AS - in Spanish)***

### MADRID KUMFUATA SANCHO

REAL Madrid itaingia vitani na Manchester United kujaribu kumsajili winga wa England, Jadon Sancho, 20, ambaye anaichezea Borussia Dortmund ya Ujerumani. ***(Star)***

### DEMBELE KUBAKI BARCA

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Ousmane Dembele, 22, anajiandaa kubaki Barcelona wakati huu kukiwa hakuna klabu iliyopo tayari kufika dau la pauni milioni 52.3 zinazohitajika na klabu hiyo ya Hispania. ***(Marca)***

### RAKITIC AICHANA BARCA

KIUNGO wa Croatia, Ivan Rakitic, 32, ameikosoa Barcelona namna inavyomchukulia na kueleza kwamba alikata kujiunga na PSG mwaka jana kama sehemu ya kukamilisha mpango wa mshambuliaji Mbrazil Neymar, 28, kurejea Nou Camp. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### SPURS KUMSAJILI BOGARDE

TOTTENHAM Hotspur ipo tayari kumsajili kiungo Mholanzi Lamare Bogarde, 16, kutoka Feyenoord. ***(Football Insider)***

Michezo
Jumatano Aprili 15, 2020
Nipashe



Solskjaer, Pep vitani kwa Upamecano UKURASA 22

KIMENUKA...



Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, ambaye ameisababishia klabu hiyo kutaka kuburuzwa FIFA na Simba. **PICHA: MAKTABA**

## Mkwasa kubeba mikoba ya Eymael

**Na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Mbelgiji Luc Eymael, akieleza ameshindwa kurejea nchini baada ya Serikali ya Tanzania kuzuia ndege zote kutoka nje kutua nchini kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19), uongozi wa klabu hiyo umesema msaidizi wake, Boniface Mkwasa, atabeba mikoba hiyo endapo ligi itarejea.

Akizungumza na mwandishi wetu jana kutoka Ubelgiji, Eymael alisema wakati huu ambao kila kitu kimekwama, wachezaji wake wanapaswa kuzingatia zaidi mafunzo binafsi ili kujiweka fiti na kuwa tayari kwa mechi wakati janga la corona litakapomalizika. Eymael alisema kutokana na hali ya dunia ilivyo kwa sasa, amekwama kurejea nchini mapema ili kuwa karibu na wachezaji wake wakati huu wakifanya mazoezi binafsi.

"Kwa sasa viwanja vya ndege Tanzania vimefungwa, hatuna namna zaidi ya kuahirisha kurudi, pole kwa hilo mashabiki wa Yanga pia wachezaji, wanatakiwa kuzingatia," alisema kocha huyo.

Alisema hali itakapotulia na mipaka kufunguliwa, lengo lao ni kufanya vizuri katika mechi zilizosalia na zaidi kwenye Kombe la FA ili kupata nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa.

Hata hivyo, juzi ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema kama ligi itarejea kabla ya mipaka kufunguliwa, kikosi chao kitakuwa chini ya Mkwasa hadi hapo Eymael atakaporudi.

# Simba kuiburuza Yanga Fifa

## ●●● Ni baada ya Mwakalebela kulikoroga kwa Chama, huku Mzambia huyo akisema...

**Na Somoe Ng'itu**

UONGOZI wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, unajiandaa kuishitaki Yanga kwa Shirikisho la Soka duniani (Fifa), kutokana na klabu hiyo kupitia kwa Makamu Mwenyekiti wao, Frederick Mwakalebela kufanya mazungumzo na kiungo wao, Clatous Chama, ambaye bado ana mkataba na Wekundu wa Msimbazi hao, imeelezwa.

**Kauli hiyo ya Simba imetolewa baada ya Mwakalebela kunukuliwa na vyombo mbalimbali vya habari juzi na jana kuwa wameanza mchakato wa kumnasa kiungo huyo wa kimataifa kutoka Zambia kwa madai mkataba wake umebakiza miezi sita tu na vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.**

Mwakalebela alitoa kauli hiyo baada ya Ofisa Mtendaji wa Simba, Senzo Mazingisa, kuweka hadharani dau la Dola za Marekani 350,000 kwa klabu inayotaka kuvunja mkataba na nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Zambia (Chipolopolo), baada ya kuibuka tetesi kuwa Yanga inamhitaji.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema Chama ana mkataba na klabu hiyo ambao utamalizika ifikapo Julai mwakani na kwamba kitendo alichokifanya Mwakalebela, amevunja kanuni za usajili za Fifa, ambapo Shirikisho la Soka nchini (TFF) ni mwanachama.

Manara alisema Simba haitakaa kimya kuona viongozi wa klabu nyingine wanawaingilia katika kuwarubuni wachezaji wao na wanaamini kwa kosa la makusudi alilofanya Mwakalebela itakuwa fundisho kwa wengine.

"Kitendo hiki ni sawa na kunajisi sheria [za Fifa], tunataka iwe fundisho, kile kilichowatokea Yanga kwa kumtambulisha Kessy (Hassan) hadi wakatulipa Simba Sh. milioni 50, haijawa fundisho, safari hii itakuwa fundisho maana Mwakalebela ni kiongozi mzoefu, hatukutegemea kufanya hili kutokana na kufahamu vema kanuni," alisema Manara.

Alisema Simba iliwaongezea mikataba wachezaji wake mbalimbali mwaka jana baada ya ripoti ya benchi la ufundi kuwahitaji na hiyo ilitokana na nyota hao akiwamo Chama kuisaidia timu hiyo kufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Manara alisema endapo Chama ataondoka Simba haitapepesuka kwa sababu ina viungo wengine wazuri ambao baadhi yao hawajapata nafasi ya kucheza kutokana na vita ya kuwania namba iliyopo.

"Tunajua maana ya usajili, tunajua maana ya kikosi kipana, Simba ina macho mapana, kwa sababu tunajua tutacheza mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, hilo halina shaka,...Yanga hawana ubavu wa kumlipa mshahara Chama, labda kidogo Azam, alitupa pesa nyingi tulipoingia makundi na baadaye robo fainali," Manara alisema.

Katika hatua nyingine, Chama aliweka wazi yeye bado anaendelea kuitumikia Simba na ndio klabu pekee ambayo anaweza kuichezea hapa nchini.

**BILIONI 20 ZA MO**

Manara alisema kiasi hicho cha fedha bado hakijawekwa katika akaunti ya klabu kwa sababu ya kutokamilika kwa mchakato wa mabadiliko ya mfumo wa uendeshaji na kufungua kampuni (Simba Sports Club Limited).

Alisema kwa sasa fedha hizo zimewekwa katika akaunti maalumu (fixed account) ya Mo na kwa makubaliano yaliyofikiwa na Bodi ya Wakurugenzi ambayo mwekezaji huyo ni mwenyekiti wake, kila mwezi anatoa kiasi cha Sh. milioni 165 ili kusaidia shughuli za kiutawala za klabu.

Alisema mchakato huo ambao unatakiwa kufuata taratibu na sheria za nchi, unaelekea kukamilika na hivi karibuni fedha hizo zitaingizwa kama ilivyokubaliwa.

"Kwanza Simba tunapaswa kupongezwa hadi hapa tulipofika, tumekaribia kufikia asilimia 90 ili kumaliza hili, wenzetu walishajaribu kufanya hivi zaidi ya mara tatu wakashindwa, walianzia mwaka 1994 kupitia kina marehemu Mpondela (George), Tarimba Abbas, hakuna ujanja kwenye suala hili na kama ungekuwapo, bwana mkubwa asingelikalia kimya, Simba ni taasisi kubwa na ya watu wengi," Manara alisisitiza.

Aliongeza mafanikio ya Simba katika mabadiliko haya, yatafungua njia kwa klabu nyingine za ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >